

KWA NINI?



Asante, Ndugu.

² Mnaweza kuketi. Mnajua, mimi...Mke wangu alisema, “Bill, kwa namna fulani ninapendezewa nawe kwenye mkutano huu, unaposhuka kwenda Texas ambako kuna hali hiyo yote nzuri ya hewa.”

Muda mfupi uliopita nilimpigia simu, nikasema, “Kuna baridi kiasi gani?”

Akasema, “Sio baridi sana, ni karibu sufuri. Lakini ninyi nyote mnafanya nini huko chini?”

³ Nikasema, “Mvua inanyesha tu na theluji inaanguka sana iwezavyo.” Nikasema, “Majira ya kiangazi hapana shaka yalienda magharibi, kwa likizo yake.” Hakika yamehamia se—sehemu ya chini ya Texas, sivyo? Ninaona ya kwamba tuna safari yenye utelezi, wa mvua kesho, na kwa hiyo tunahitaji maombi yenu.

⁴ Wala sikutarajia kungekuwako na mtu yeyote huku nje, nilifikiri Texas ililogopa hali mbaya ya hewa, lakini naona baadhi yao hawaogopi. Kwa hiyo, kwa hiyo tuna furaha kwamba mko hapa usiku wa leo, na tuna furaha kwamba tulikuwa na huu, mlitonyesha mkutano huu mzuri sana, mmoja wa mikutano mizuri sana ambayo tumekuwa nayo kwa miaka mingi, roho yenu nzuri na ushirikiano.

⁵ Ninataka kuwashukuru wachungaji hawa, kila mmoja wenu, kwa ushirikiano wenu mwema. Sikupata kula chakula cha jioni pamoja nanyi, nilikula tu kiamshakinywa pamoja nanyi nyote. Lakini ningetaka kwenda huko nione jinsi mke wako anavyoweza kupika sambusa na biskuti, na, loo, jamani, ninawazia ingekuwa sawa, ingekuwa nzuri. Ninamthamini maskini mpiga kinanda wetu hapa ambaye amekuwa mzuri sana, akitusaidia, ninyi watu wote.

⁶ Nao wananiambia ya kwamba walitoa sadaka ya upendo katika, kwa ajili ya...kwa ajili yangu. Hivi gharama zote zimelipiwa, ndugu? Kama sivyo, itumieni moja kwa moja kwa hizo, mnaona. Na kama kila kitu ni sawa, wala hakuna haja yake maalum, nitaiweka katika kazi ya Bwana, ninaposafiri. Mungu na awabariki daima.

⁷ Nami naamini imesemwa katika Maandiko, “Kadiri mlivyomtendea aliye *mdogo kuliko wote* wa watoto Wangu, mmenitendea Mimi.” Kwa hiyo mimi ndiye huyo aliye mdogo kuliko wote, kwa hiyo mmentendea Yeye, mnaona, [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...mlimtendea. Ninajua ni sehemu ya riziki yenu, mnashiriki nami kwa ajili ya Injili. Ninaomba

ya kwamba Mungu atawabariki sana, kwamba maisha yatakapokwisha hapa, kwenye Ng'ambo ya pili mtapewa thawabu, kama si hapa, mara mia moja hapa, na Uzima wa Milele kwenye Ng'ambo ya pili.

⁸ Imani yenu imekuwa kubwa sana, jinsi ambavyo mmekusanyika pamoja na kushikilia imani yenu, mkiunganisha imani yenu. Kama isingalikuwa ni kwa ajili ya imani hiyo, huu mkutano usingalikuwa jinsi ulivyo, bali ni kwa sababu mmeamini, na kuamini pamoja nami, nami na—nathamini hilo. Niliwaambia ndugu zangu, na kuwaambia marafiki ambao wamenipigia simu kutoka sehemu mbalimbali za nchi kwamba ulikuwa ni wa ajabu sana, jinsi ambavyo wa—watu hapa Beaumont hakika wameweka imani yao na maombi nyuma ya huu mkutano, na kusaidia.

⁹ Hapana shaka kwamba kila kitu, wakati kinapofanya ninii ndogo, historia ndogo, ama tu kitu kisicho cha kawaida, una ubaya na uzuri wake, una me—mema na mabaya. Huna budi kuwa na usiku upate kuufurahia mchana, huna budi kuwa na hali mbaya ya hewa upate kufurahia hali nzuri ya hewa, hivyo ndivyo maisha yalivyo. Hatuna budi kuwa na watu wabaya kuwafanya watu wazuri waonekane. Na kwa hiyo, inatubidi kuwa na ya bandia kufanya yaliyo halisi.

¹⁰ Sisemi hili ati kwa sababu niliambiwa niliseme, ninalisema kwa sababu linatoka moyoni mwangu, nami ninataka kuwaambia, ninyi watu wote, ninyi makanisa, nisingewataka mfikirie kwamba nilikuwa m—mtu aliyekaribu kupingana na makanisa yote, na ati, “Wote wamekosea, na mimi ndimi niliye sahihi.” Kama nimeacha wazo hilo, samahani, sikulimaanisha hivyo. Lakini nilimaanisha kusema ya kwamba hakuna dhehebu ulimwenguni, siamini, la dini ya Kikristo lisilo na watu wazuri ndani yake, nayo yana watu wa Mungu ndani yake.

¹¹ Sikubaliani na madhehebu, mimi, kwa sababu kwamba madhehebu, sasa sikilizeni kwa makini, kama dhehebu likisema, “Tunaamini *hili*,” na koma, vema, lakini kama, “Tunaamini *hili*, kikomo,” hayo yote ni makosa, mnaona. Mnaona? Kama ukimalizia fundisho lako kwa koma, “Tunaamini *hili*, pamoja na kadiri Mungu anavyotaka kuliongezea,” lakini mnaposema, “Tunaamini *hili*, kikomo, na ni hivyo tu,” basi papo hapo mnamfungia Mungu nje. Mnaona? Na hivyo ndivyo madhehebu yanavyofanya, yanamalizia kwa—kwa kikomo.

¹² Sasa, mambo kama hayo yalitukia kwa mmoja wa ndugu zetu, kwa sababu kwamba alikuwa ameomba kwa miaka mingi, naye alikuwa ameomba nipate kuja hapa. Nami nataka kuwaambia jinsi Bwana alivyotenda kazi. Nilikuwa na malundo makubwa ya mialiko, ulimwenguni kote. Mimi huweka uamsho wangu wote wa Marekani pamoja, halafu wangu wa kigeni, wa ng'ambo mwanzoni mwa kila mwaka. Ninaanzia kwenye juma

la Krismasi nasi tunaomba juma zima, maana kwa kawaida sisi huwa nyumbani wakati huo.

¹³ Na—na kwa hiyo tukaliombea, na papo hapo mawazo yangu yakavutiwa kwenda Texas, Houston, ama, si Houston, bali Beaumont. Halafu katika . . . Nikasema, “Mna chochote kutoka Beaumont?”

¹⁴ Katibu akaleta mialiko, kadhaa, nami nikasema, “Hebu tuone.” Ndipo nikachukua moja tu namna *hiyo*, nikaiweka, nikachagua moja, ndipo nikaona jina la maskini mchungaji huyu, nikasema, “Wasiliana naye.” Mnaona, “Hebu wasiliana na Ndugu.”

¹⁵ Halafu basi, huyo ndugu, akiwa na nia njema, bila hisia mbaya . . . Na kama baadhi ya watu wa hili jimbo wapo hapa, wazee wa jimbo, ama chochote kile, ndugu, msifanye uovu ambao mtaujutia baadaye. Mnaona? Mnaona? Kuwa Mkristo, kuwa mwungwana. Maskini huyo ndugu hakutaka kudhuru, alikuwa tu akijaribu kufuatilia, naye alishukuru kwa ajili ya maombi kujibiwa, hivyo tu. Hivyo tu ndivyo ilivyokuwa, kushukuru tu kwa ajili ya Mungu kujibu maombi yake. Hakumaanisha kuwa mwovu, naye, sidhani ndivyo alivyo, yeye ni ndugu mwema, ndugu mzuri, mpole.

¹⁶ Halafu basi wakati ndugu yake mwema, mmoja wa . . . Yeye ni wa UPC, ambalo linaitwa miongoni mwa watu, *Umoja*. Ndipo baadhi ya ndugu waaminio wa utatu wakaingia. Moyo wake una njaa ya ushirika, na wakati ndugu yake wa utatu alipokuja, alikuwa ni nini, hakuna la kufanya, ila kumkumbatia. Sasa, ndugu, kama mkimtenga mtu kutoka kwenye makusanyiko yenu kwa ajili ya kitu kama hicho, Mungu na airehemu nafsi yenu yenye dhambi! Ninapofika mahali fulani, ama shirika lolote ambalo haliwezi kunyosha mikono yake na kumkumbatia ndugu kutoka mahali popote, Mungu na awarehemu!

¹⁷ Ndugu wa Assembly, nanyi Church of God, Foursquare, na ninyi nyote, nina hakika mnaweza kuthamini msimamo ambao ndugu shujaa angechukua namna hiyo. Nina hakika kwamba ninyi ndugu wa Assembly mnathamini hilo, ninyi Foursquare, na Church of God, na ndugu wanaoamini utatu. Ndugu huyu aliunyosha moyo wake, hakuwa na moyo wa kusema, “Kaeni mbali,” kwa sababu anawapenda. Sasa, wakati akiwa katika sehemu yake wakati amedhoofika, akilazimika kujikaza sana, na kutegemea hilo wakati wote, kama jambo lolote lingetukia na ndugu wamfukuze kwenye dhehebu kwa sababu ati alishirikiana nanyi, kumbukeni hilo.

¹⁸ Fanyeni ushirika mmoja na mwingine, na msahau tofauti zenu ndogondogo, muwe ndugu ninyi kwa ninyi, na kumwimarisha, kumsaidia, na kumpigapiga mgongoni, na kusema, “Njoo, Ndugu, tuko pamoja.” Hiyo ndiyo njia ya kufanya hilo, hiyo ndiyo njia ya kulifanya. Utaona jambo moja,

ndugu, ukosoaji utakuingiza tu katika shida. Hiyo ni kweli. Kamwe usimshushe mtu yeyote, wainue juu.

¹⁹ Nitasimulia hadithi ndogo kuhusu hili, imekuja tu akilini mwangu. Hakuna wengi hapa usiku wa leo, kwa hiyo tuna wakati mzuri wa kuzungumza, tutawaombea wagonjwa, niwape ujumbe wangu mdogo wa kuwaaga. Nami ningetaka kusema ya kwamba hapa wakati fulani uliopita nilikuwa Ohio, tulikuwa na mkutano mkubwa, imekuwa kama miaka minne au mitano iliyopita, labda sita. Nao mkutano ukawa mzito sana hata ikanibidi kuhamia mashambani, ile moteli ndogo nilimokuwa nikikaa, wengi sana walikuwamo, ama, hoteli, hasa, nikahamia mashambani. Nilikuwa nikifunga kusudi jambo fulani maalum litukie, ambalo, jambo ambalo lingejutia mioyo ya watu.

²⁰ Mnajua, wakati mwingine tunapowaombea wengine, sisi ndio tunaopata msaada mara nyingi wakati unapowaombea wengine, kama vile usiku ninaposema, “Wekeaneni mikono, usijiombe mwenyewe, bali mwombe huyo jamaa mwingine, yeye anakuombea. Biblia ilisema, ‘Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana.’”

²¹ Hivyo ndivyo tunavyotaka kufanya. Hebu Wabaptisti wawaombe Wamethodisti, na Wamethodisti wawaombe Wabaptisti, na wa Umoja wawaombe wa Uwili, na wa Uwili wawaombe wa Uwili, na wa Utatu, na wa Unne, na wowote wale wanaokuja. Kila mtu amwombe mwenzake, kusudi imani yetu isishindwe katika Yule mmoja mtukufu ambaye sisi sote tunampenda, Yesu Kristo. Naam, bwana.

²² Sasa, kwa hiyo nikahamia mashambani, yapata maili tatu nje ya mji. Na kwa hiyo tulikuwa, tulikuwa tukila chakula cha jioni kwenye mkahawa mdogo wa Dunkard ambapo ninii, ninaamini ilikuwa ni Wamenoni, nao walikuwa ni kundi zuri la watu wanaoamini katika utakatifu. Na maskini hao wasichana, wamevalia vizuri tu na watauwa, huku maskini ninii zao, huku nguo zao zimewaenea vizuri, na nywele ndefu, na safi kama pini; nilipenda tu kula huko. Nao walikuwa wakihudhuria mkutano wangu, nasi tulikuwa tu na wakati mzuri sana. Kwa hiyo, Jumapili walifunga mahali pale padogo, walikuwa kwenye mkutano, na hasa sana Jumapili hawakufungua.

Kwa hiyo, nilikuwa nimefunga kwa yapata siku mbili ama tatu, nami nilikuwa tu niende kuhubiri alasiri hiyo, nikawaza, “Vema, inaonekana kama . . .”

²³ Kamwe usitamani kufunga mpaka uongozwe kufunga, halafu kama ukiona njaa, ni wakati wa kula. “Baadaye, *baadaye* Yesu akaona njaa.” Baadhi ya hawa wanaosema, watu hawa wanaofunga, na kusema, “Nitafunga siku arobaini,” huku meno bandia yakianguka, na kupungua uzito, na, jamani, afadhali mwachane na hilo. Ngoja mpaka Mungu akuongoze kufanya hivyo juu ya mambo hayo. Ongoza na Roho.

²⁴ Nimekuwa na watu, baada ya kitabu fulani kuandikwa na kutolewa kuhusu kufunga, watu huingia kwenye mstari wangu, wanawake, wajawazito, na kadhalika, wanakuja kwenye mstari wangu, wamerukwa na—wamerukwa na akili, wanapelekwa katika hospitali ya wendawazimu kutokana na hilo. Mnaona? Bila shaka huwezi kufanya hivyo. Ati kwa sababu tu mtu mwingine alifanya hivyo, hiyo si ishara kwamba unapaswa kufanya hivyo, acha Mungu akuongoze kufanya yale unayofanya.

²⁵ Unapoongozwa, ukiona njaa, ni wakati wa kula. Mungu anapoweka kufunga juu yako, huoni njaa, ni Mungu akikushughulikia. Yesu *baadaye* aliona njaa. Unaona? Baada ya kufunga Kwake kwisha, aliona njaa. Lakini, kwa hiyo hata hivyo, acha tu hilo—hilo... Wewe jiamulie tu hilo, mimi... Mchungaji wenu anafaa zaidi... nafasi bora zaidi ya kuwaambia mambo hayo. Kama nilisema vibaya, ama, kunradhi.

²⁶ Lakini hata hivyo, nilikuwa nimefunga kwa siku chache, au tatu, ambazo ni kadiri ya muda ninaoweza kufunga, kwa sababu nina shughuli nyingi sana. Kwa hiyo basi nikawazia, “Vema, nitahubiri tu alasiri ya leo, kwa hiyo nitaninii tu, nitaenda kule nikajinunulie sambusa.” Kisha nikawazia, “Loo-loo, wamefunga.”

²⁷ Huko upande wa pili wa njia kulikuwa na ninii, mkahawa mdogo tu wa kawaida wa Marekani, wa kawaida. Vema, niliingia tu mle polepole wakati walipokuwa wakifanya utangulizi. Nikawazia, “Nitajinunulia tu hambaga, na hiyo kidogo itaondoa makunyanzi mpaka niweze, usiku wa leo nitakula baada ya ibada.”

²⁸ Kwa hiyo basi, nikachukua ninii yangu... nikaenda kununua hambaga. Nami nikatembea mahali hapo, basi nilipoingia mahali hapo, mazingira yenyewe, ungeweza kujua hukuwa miongoni mwa waaminio. Upande wa kushoto kulikuwa na mtambo wa kamari, na polisi amesimama pale, huku, yapata umri wangu, huku amemkumbatia mwanamke, akicheza kamari.

²⁹ Sasa, kucheza kamari ni haramu Ohio, naye huyu hapa akicheza kamari, mtu aliyepaswa kulinda sheria, akivunja sheria. Na mtu aliyepaswa kuwa, kutoa mfano wa maadili, na kadhalika, na huku amemkumbatia mwanamke, ambapo hapaswi kugusa, na ni mwanamume wa rika yangu! Vema, yeye, nakisia alikuwa ameo na alikuwa na familia, sijui mimi. Ndipo nikawazia, “Jamani!”

³⁰ Nikaangalia nyuma, na kulikuwa na kundi la wavulana hawa mezani, hao jamaa wa pikipiki wenye mtindo huo wa kukata nywele kibata, na majaketi ya pikipiki, na ovaroli zilizoshushwa nyongani mwao, ama... Chochote... Wanahitaji baba mzuri kweli wa kusini, wa mtindo wa kale, mwenye fimbo

ya hikori yenye zile Amri Kumi nchani mwake. Hilo ndilo hasa wanalohitaji. Naam. Mnaita...Ni nini kilichowapata Wamarekani? Mnajua nini? Wanauita uhalifu wa watoto, nafikiri ni uhalifu wa wazazi, hiyo—hiyo ni kweli kabisa. “Usipotumia fimbo utamharibu mwanao.” Hivyo ndivyo Maandiko yasemavyo.

³¹ Nao hao hapo wameketi kule nyuma, na msichana, mrembo, msichana mdogo, na mvulana mmoja amesimama pale, kwa namna fulani ndiye kiongozi wa hilo kundi, huku buti zake zikiwa juu ya meza, na mkono wake umemkumbatia msichana huyo ambapo ilikuwa ovu sana kwenye nyonga zake, namna hiyo, na kumkumbatia huyu mhudumu mikononi mwake. Vema, nilisimama pale, nikawaza, “Masalaale!”

³² Nikaangalia upande *huu*, na hapo aliketi maskini bikizee, yapata rika ya nyanya yangu. Naye, maskini huyo bikizee alikuwa amevaa nguo hizi zinazobana, ama kaptura, ama vyovyote mnavyoziita, na maskini mikono yake mizee, nyama teketeke, naye alikuwa amepaka rangi kucha za vidole vya miguu yake rangi ile ile ya midomo yake, na madoa makubwa mno meusi chini ya macho ya—yake hapa ambapo alikuwa amejipaka kitu fulani, nazo nywele zake zilikuwa zimepakwa rangi ya bluu. Sasa, mnajua wanadamu angalau hawana hiyo bluu ya kijani kibichi. Kwa hiyo, nikawaza, “Vema, maskini bikizee! Labda hilo ni sawa, labda anapenda hilo.”

³³ Lakini nikaangalia, naye alikuwa pamoja na jamaa wawili wazee, nao walikuwa wamelewa. Na mmoja wao, papo hapo katika msimu wa kiangazi, alikuwa amevaa maskini kabuti kubwa la kijeshi, huku amejifunga skafu kubwa shingoni mwake. Nao walikuwa na bia imewekwa mezani.

Nikawaza, “Loo, kamwe sitakula hapa ndani hata iweje!”

³⁴ Kwa hiyo, nikawazia, “Mungu, unawezaje, ukiwa mtakatifu, kuangalia kitu kama hicho?” Nikawaza, “Hivi mtoto wangu Sarah na Rebekah itawabidi kuja chini ya upuuzi kama huo kama Wamarekani?” Wasichana wangu wawili wadogo ninaojaribu kuwalea kwa ajili ya Mungu wawe wamishenari, ama wapiga piano, ama chochote kile, labda aolewe na maskini mhubiri ambapo atamsaidia katika kazi ya Bwana, kujaribu kuwalea wasichana safi na wenye haki, wawe wanawake halisi, nao inawabidi kupitia chini ya mazingira kama hayo!

³⁵ Nikasema, “Baba, kwa roho niliyo nayo, ambayo Wewe ulinipa, roho yangu ikitakaswa na ninii Yako, Damu ya Mwanao, na hilo linaonekana ovu kwangu, unawezaje Wewe kuvumilia kuliangalia? Mbona usipige tu kitu hicho na kukiondoa duniani!” Huenda hasira yangu ya haki ilipanda. Mnaona? Hatutaki kusema ilikuwa ni hasira, bali ilikuwa tu kitu fulani, ilikuwa ni aina ile ile ya hasira aliyokuwa nayo Yesu wakati

alipowaangalia kwa hasira na kuwapiga watoke hekaluni, mnaona.

³⁶ Na kwa hiyo, niliangalia kote na kuona hayo yote, nami nikawazia, “Na mtoto wangu Sarah, Rebekah itabidi apitie chini ya kitu kama hicho? Mungu, inaonekana kana kwamba ukiwa ni mtakatifu, na jinsi ulivyo mkuu, inaonekana kana kwamba ungekilipulia tu mbali kitu hicho kutoka kwenye ramani, namna hiyo! Ungewezaje kukistahimili?” Nikawaza “Loo, jamani!”

³⁷ Ndipo nikasikia kitu fulani kikienda, “*Whiu, whiu, whiu,*” kama kuchapwa. Hivyo ndivyo Nuru hiyo wakati inapotokea, inavuma kama moto. Nami nikaona, na ilikuwa imesimama karibu nami. Nikarudi nyuma ya mlango. Nikakiegemeza kichwa changu ukutani, kisha nikasema, “Baba wa Mbinguni, nini...?” Nikawazia... Sasa, hivi ndivyo nilivyokuwa nikiwazia. “Je, unataka niitisha Hukumu?” Sasa, hiyo inaonyesha tu jinsi mwanadamu anavyoweza kwenda mbali sana.

³⁸ Nikarudi nyuma. Nilifikiri alikuwa akitaka kuniagiza niende tu huko nje na kusema, “Ninyi nyote, ninamkemea kila mtu, enyi wenye dhambi! Tubuni la sivyo mfe!” Mnaona? Nami nilifikiri hivyo ndivyo Yeye angeniambia nifanye; nisingefanya hivyo isipokuwa Yeye aniambie. Kwa hiyo ni—nikatoka, nikarudi kule, nami nilifikiri Yeye alikuwa anaenda kunionyesha.

³⁹ Nilipofanya hivyo, niliona, ilionekana kama, nilipoyafungua macho yangu baada ya kujua Yeye alikuwa pamoja nami hapo nyuma ya mlango, na ilionekana kama kitu kinachozunguka. Nikaanza kuangalia, na ilikuwa ni ulimwengu, dunia hii, nayo ilizungukwa na ukungu, kama ukungu mwekundu ukivuma pande zote, nikaangalia huko juu kabisa, ndipo nikamwona Yeye.

⁴⁰ Kisha nikaangalia chini, nikajiona, ilionekana kana kwamba nimekuja moja kwa moja duniani. Na kila kitu ambacho ngingefanya kilikuwa kibaya, dhambi yangu ingeenda kukutana na Mungu. Na kabla haijamfikia, Yesu alitenda kama bamba kwenye gari kati yangu na Mungu. Mnaona? Ilimgonga, Naye angeushikilia ubavu Wake, machozi yangetiririka kutoka machoni Mwake, nami ningemsikia akisema, “Baba, msamehe, hajui atendalo.”

⁴¹ Nikajiangalia kama mvulana mdogo, mambo niliyofanya. Nami ningeona kila wakati ngingefanya kitu kiovu, mbona, ilionekana kana kwamba kingepaa juu, naye Mungu angeniua kwa ajili yake, mnaona, nami, maana Yeye ni mtakatifu, dhambi haiwezi kusimama Mbele Zake, bali niliona ukungu huo ukivuma pande zote, na hiyo, hiyo Damu ya Yesu, inatenda kama bamba kati yangu na kuuawa na Mungu.

⁴² Vema, nikaangalia, nikakaribia mahali alipokuwa, nami nikaangalia, na hicho hapo kitabu changu kimewekwa mbele

Zake, na mle ndani mlikuwamo na jina langu, na kila jambo baya nililowahi kufanya liliandikwa moja kwa moja juu yake. Basi nikaona kila wakati ambapo ningefanya jambo baya, ku-... Nilipolitenda, Yeye ange—Yeye angelishika, nalo li—lilimwudhi, Naye angezuilia pumzi Yake, na machozi yangetiririka mashavuni Mwake, Naye angesema, “Msamehe, hajui atendalo.”

Nikawaza, “Bwana, kwani nilikufanya uteseke hivyo?” Nikawaza, “Nakupenda! Hivi ningekufanya uteseke namna hiyo? Unamaanisha dhambi zangu zilifanya hivyo?”

⁴³ Akaniashiria kwa kichwa Chake, nami ningeweza kuona hiyo, alionekana kama mnavyomwona kwenye picha, amevaa ile taji, namna hiyo, Damu machoni Mwake na usoni. Akaniangalia, na ilionekana kama machozi yalisokota ndevu Zake pamoja, amejaa madoa ya Damu kote usoni Mwake.

Nikasema, “Hivi dhambi zangu zilikufanyia hivyo?”

Akaniashiria kwa kichwa Chake.

Nikasema, “Mungu, nisamehe. Ni—nisingetaka—nisingetaka kukuumiza namna hiyo, Bwana. Ninakupenda kwa moyo wangu wote.”

⁴⁴ Akachukua ubavu Wake, akaupigapiga kwa mkono Wake, akainua kidole Chake namna *hii*, na kuandika kwenye maskini kitabu changu kichafu, “Amesamehewa,” akakichukua na kukitupa nyuma Yake, namna *hii*, katika Bahari ya Usahaulifu, akatoa kitabu kipya.

Nikasema, “Bwana, ninakushukuru. Sita—sitajaribu kamwe kufanya jambo lolote baya. Wewe. . .”

Akasema, “Sasa, nilikusamehe bure, nilikusamehe bure, halafu wewe unataka kumwangamiza.”

⁴⁵ Na kufikia wakati huo mlango ulikuwa umerudi tena, nami nilikuwa nikimwangalia moja kwa moja yule mwanamke aliyeketi pale. Nilitaka kumwangamiza, baada ya mimi kusamehewa bure. Nikaufungua tu mlango tena ambapo nilikuwa nikisogeza mikono yangu wakati ono likiendelea, nikaufungua mlango, nikasema, “Baba, nisamehe. Ni—nitamwendea mara moja na kuomba msamaha.”

⁴⁶ Nikatoka nje ya mlango. Mmoja wa hao wazee, amelewa, ameketi pale pamoja naye, kasema, “Unafikiri mvua itaidhuru rubabu?” Ndipo wakaamka, na wakaomba waondoke, wakatoka nje, kwenda msalani.

⁴⁷ Kwa namna fulani nikatembea huku na huku, huku polisi huyu angali anacheza kamari. Nami nikaenda kwa namna fulani mahali alipokuwa, nikasema, “U hali gani?”

Maskini bikizee akainua macho na kusema, “Loo, halo.”

Nami nikasema, “Naweza kuketi chini?”

Akasema, “Asante, nina mwenzangu.”

Nikasema, “Sikumaanisha hivyo.” Nikasema, “Ninataka tu kukwambia neno moja. Nataka uulize kama... ninataka kukuomba unisamehe.”

Kasema, “Uliwahi kunifanyia nini?”

Nikasema, “Waweza kusubiri kidogo tu, uniache nikwambie?”

Kasema, “Ndiyo.”

Nikasema, “Nilisimama pale mlangoni,” nami nikamsimulia hadithi hiyo. Nikasema, “Moja kwa moja huko nyuma, Yeye alinionyesha mahali nilipokosea.”

Akaangalia juu, na ilionekana kana kwamba ilimtoa ulevi, akainua macho yake, akasema, “Wewe ni Ndugu Branham?”

Nikasema, “Naam.”

Akasema, “Wewe ndiye yule mhudumu hapa chini.”

Nikasema, “Naam, mama.”

Akasema, “Ninaona aibu kwako kuniona namna hii.”

Nami nikasema, “Utanisamehe?”

Akasema, “Bila shaka.”

Akasema, “Keti chini.”

Nikasema, “Asante.” Nami nikaketi kwenye hicho kibanda kidogo pamoja naye.

⁴⁸ Naye akasema, “Ninataka kukwambia jambo fulani, Ndugu Branham.” Akasema, “Nilipita na kuona mikutano yako, niliiona imetangazwa, nikaingia.” Kasema, “Ninajionea tu aibu.” Akasema, “Ungeamini nini kama nikiwambia kwamba baba yangu alikuwa mhudumu wa Kimethodisti?” Kasema, “Nina binti wawili, wote wawili ni walimu wa shule ya Jumapili.”

Nikasema, “Ilikuwaje?”

⁴⁹ Akaniambia kuhusu ba—barua kutoka kwa mumewe, naye alitoroka na mwanamke mwingine, akaanza kunywa pombe, akaanza kwenda, naye akasema, “Ninajua si—sikomboleki,” mshika sheria kabisa, mnaona. Nami nikasema... Kasema, “Sikomboleki.”

Nikasema, “La, sivyo. La, sivyo.”

Akaanza kulia, akasema, “Ndugu Branham, unafikiri sijapita ukombozi?”

⁵⁰ Nikasema, “Kwa nini Yeye akaniambia hivyo basi, dakika chache zilizopita?” Nikamshika mkono, nikapiga magoti pale sakafuni, na hapo akampa Yesu Kristo maisha yake. Nena kuhusu hiyo mitambo ya kamari kusimama na kadhalika! Kila

mtu mle ndani, alikuwa akilia na kuomba. Akasimama, akatoka kwenda nyumbani, maisha mapya.

⁵¹ Mnaona, Mungu alinionesha ya kwamba moyo wangu mwenyewe haukuwa sawa, kwa sababu nilikuwa nikijaribu kumhukumu, na bila kuangalia ninakotoka, pia. Kwa hiyo kama daima tunaweza kukumbuka, kuangalia nyuma kwenye shimo tulimochimbuliwa, mambo yataonekana tofauti sana. Mnaona? Hatutaki kumhukumu mtu yeyote, mpende kila mtu.

⁵² Kila unapopoteza upendo huo halisi, wa kweli ulio moyoni mwako, umepoteza kila kitu, unaona. Kamwe usisahau jambo hilo, kwamba unapopoteza upendo, yote yamekwisha.

⁵³ Sasa, kumbukeni hilo, upendo aliokuwa nao maskini ndugu huyu kwa ajili yenu nyote. Nasi tutakumbuka upendo wa ndugu hapa.

⁵⁴ Ndugu, chochote ufanyacho... Sisemi ninyi madhehebu yote msambaratike na kuunda dhehebu moja, haitakuwa hivyo kamwe. Kamwe hamtafanya hivyo, mtapitia tu maishani maskini kitu kile kile kikigonga, na kuzozana, na kushikwa na hamaki, hivyo ni vibaya. Dumisheni dhehebu lenu, kaeni humo mkiweza, hilo ni sawa, bali nyosha mkono, na umpende kila mtu, na uwe na heshima. Mpe blanketi kidogo, pia, kwa sababu anataka kujifunika, pia, itaenea vya kutosha kwa ajili yetu sote.

Nafasi, nafasi, kuna nafasi tele.

Kuna nafasi kwenye chemchemi kwa ajili yangu.

Hiyo ni kweli, kuna nafasi kwa ajili yetu sote, basi kumbukeni tu hilo.

⁵⁵ Kama ningeweza kuona kila kanisa la Kipentekoste, Foursquare, Open Bible Standard, Pentecostal Assemblies of God, United Pentecostal Church, na hao wengine wote, wakikumbatiana, na kusahau tofauti zao, wakishirikiana tu mmoja na mwenzake, ningesema, "Mruhusu mtumishi Wako aondoke kwa amani kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu Wako." Hiyo ni kweli. Na maadamu Shetani amewafanya ninyi mrushiane risasi, yeye ataketi tu kitako na kuchukua likizo, haimbidi kujipumbaza hata kidogo, mnaona. Ninyi... Mnaona? Ninaomba ya kwamba nitaishi kuona siku hiyo.

⁵⁶ Na msipofanya hivyo mioyoni mwenu, namna fulani ya mateso yatalikumba taifa hili moja ya siku hizi, mtakuwa na shauku ninyi kwa ninyi basi, ndugu wa imani moja ya thamani. Kwa hiyo kwa nini tupitie kwenye adhabu, wakati tunaweza kuwa na sehemu ndogo ya Mbingu duniani sasa hivi? Mungu awe pamoja nanyi.

⁵⁷ Ninataka kurudi. Niliwasikia mkiuliza, mkasema mimi... mlitaka nirudi. Nitarudi siku moja, Bwana akipenda. Ningependa kuleta hema na kulipiga hapa nje mahali fulani,

katika, moja kwa moja katikati ya miji iliyo hapa, na sote tuje pamoja na kufanya ushirika sisi kwa sisi, tujaribu kuyajenga makanisa.

⁵⁸ Kila mmoja wenu ana jambo la kufanya sasa. Kila mmoja wenu ingia moja kwa moja kanisani mwako, na ufanye kazi kwa bidii uwezavyo kwa ajili ya kanisa lako la mahali hapo. Unaona? Lakini kamwe usikosoe. Kama unajua jambo baya kuhusu upande huo mwingine, usiseme lolote kulihusu, unaona, liweke hilo moyoni mwako, adui, anasikiliza tu apate kusikia hilo. Unaona? Usimwache ajue chochote, asiseme lolote huko nje, ndipo hatajua lolote kulihusu. Unaona? Liweke moyoni mwako, na uombe.

⁵⁹ Useme, “Vema, maskini ndugu huyo alifanya makosa.” Lakini usimfinyilie chini, yeye yuko chini, kwa vyovyote vile, jaribu kumwinua, unaona, kumwinua juu. Kuwa Msamaria mwema, unaona, jaribu kumwinua. Kama huwezi hata kuongea naye, mwombee mpaka iwe hivyo. Mweke tu moyoni mwako, maana nafsi yake ina thamani ya dunia elfu kumi.

Sasa na tuombe.

⁶⁰ Baba yetu wa Mbinguni, tunapotaka kuinama kukushukuru Wewe kwa ajili ya watu hawa mashuhuri hapa chini, watumishi Wako, ninakushukuru kwa ajili ya Ndugu King, Ndugu Petty, kwa ajili ya hao wengine wote, Bwana, ndugu hawa wazuri, dada hawa wazuri sana, makanisa yao, washiriki wa—wao, na kwa hao watu mashuhuri mijini, na mahali pa biashara, jinsi ambavyo wamekuwa wazuri sana.

⁶¹ Tunakushukuru kwa ajili ya ukumbi huu wa mikutano, kwa ajili ya hawa—hawa watu walioturuhusu kuuchukua. Mungu, jinsi daima wamefungua milango yao wazi kila mahali kwa ajili yangu, wakati mvua, na dhoruba, na kadhalika! Mungu, jalia waishi hata Kuja kwa Bwana. Tujalie. Wabariki wasimamizi, washiriki wote wa chama, wote. Wote na wapate raha na amani katika Kristo. Tujalie, Bwana.

⁶² Wabariki hawa polisi wazuri ambao wamekuwa wakiangalia hivi viwanja hapa nje, maskini jamaa huyo hivi majuzi usiku aliyetoka nje na kuniangalia, na kutoa sifa hizo nzuri sana. Baba, nilikuwa karibu kwisha wakati huo, nikitoka tu kwenye upako hadi kuwa... Sikuwa na nafasi ya kumwambia mengi. Kama mvulana huyo hajaokoka, na jinsi yeye, pongezi alizotoa kuuhusu huo mkutano, ninaomba, Mungu, ya kwamba atampokea Roho Mtakatifu, jalia, Bwana, awe Utukufuni. Kama kamwe sitamwona tena duniani, jalia niweze kumpa mkono. Mtu kama huyo angekuwa polisi mzuri kwa mji wowote.

⁶³ Maskini jamaa huyu niliyezungumza naye mlangoni muda mfupi tu uliopita, Mungu ambariki mtu huyo. Tunakushukuru tu kwa ajili ya kila kitu, Bwana, Wewe ni mwema sana kwetu.

Tunaomba sasa ya kwamba utaendelea kutubariki tunaposafiri kuelekea Pwani ya Magharibi.

⁶⁴ Ninaomba ya kwamba utambariki Ndugu King sasa, nasi tumezungumza juu ya shida zake, nasi tunaomba ya kwamba Wewe utakuwa pamoja naye na ndugu wengine wote. Na, Mungu, jambo pekee ninaloweza kufanya ni, mwanadamu asingeweza kulifanya, lakini naomba Roho Wako Mtakatifu sikuzote aifunge mioyo hii pamoja ya watu hawa mpaka wawe mmoja katika Kristo Yesu. Tujalie, Baba.

⁶⁵ Utupe ibada kuu usiku wa leo. Wengi wao wamepitia kwenye barabara zinazoteleza, na—na huko nje kwenye mvua hii na dhoruba kuja hapa usiku wa leo kusikia ibada ya kufunga, ninaomba ya kwamba utawabariki. Jalia kusiwe na mtu mnyonge miongoni mwetu usiku wa leo. Ninaomba hilo, Baba, kwa ajili ya utukufu Wako. Jalia nguvu za Roho Mtakatifu ziingie usiku wa leo na kutoa mengi kwa wingi sana kuliko yote ambayo hata tungeweza kufanya au kuwazia. Zaidi ya hayo tunakungojea Wewe. Katika Jina la Yesu, useme nasi. Amina.

⁶⁶ Vifurushi vyote vidogo humu ndani, mnaweza kuvichukua mara tu tunaponinii...ninapoviombea. Ninataka kungojea mpaka upako wa Roho Mtakatifu utakapokuja juu yangu kuwaombea wagonjwa.

⁶⁷ Sasa katika Kitabu cha Yeremia, kifungu cha 22:

*Je, hapana zeri katika Gileadi; huko hakuna tabibu?
mbona basi...haijarejea afya ya binti ya watu wangu?*

⁶⁸ Ninataka kuchukua somo, katika kufunga usiku wa leo, la kuuliza swali, kama Mungu alivyofanya, *Kwa nini?* Sasa, natumaini hatutachukua muda mrefu, dakika ishirini, thelathini, ndipo tunaweza kuwaombea wagonjwa. *Kwa nini?*

⁶⁹ Kama Mungu akifanya maandalizi, ama mahali pa kuepukia, halafu watu wakose kutembelea humo, Mungu ana haki ya kuuliza ni kwa nini. Hivi hamwamini hilo? Ana haki ya kuuliza ni kwa nini.

⁷⁰ Kama...Wewe huhukumiwi kwa sababu ni mwenye dhambi, unahukumiwa kwa sababu humkubali Yesu kama Mwokozi wako. Sasa, Mungu angekuwa asiye haki kukuhukumu, na asikufanyie maandalizi ya kuepukia, kwa sababu ulizaliwa katika dhambi, ukaumbika katika uovu, ukaja ulimwenguni ukisema uongo. Haidhuru wazazi wako walikuwa ni akina nani, ama walikuwa nini, wewe ungali ni mwenye dhambi tu, kama mtoto mwingine yeyote unapozaliwa katika ulimwengu huu.

⁷¹ Sote tumezaliwa katika dhambi, tusingeweza kujiokoa. Hatungeweza kujiokoa wenyewe, kuliko tungeweza kuchukua kamba zetu za buti na kujinyanyulia mwezini. Tusingeweza kufanya hivyo, hatujiwezi kabisa. Na kwa hiyo Mungu

asingekuhukumu kwa misingi hiyo kwa sababu wewe ni mwenye dhambi, Atakuhukumu kwa sababu unakataa kuchukua njia ya kuepukia. Kwa hiyo basi si Mungu, ni wewe mwenyewe, unajihukumu mwenyewe. Na unapojihukumu mwenyewe, hakuna mtu wa kukuhurumia ila wewe mwenyewe. Hivyo tu. Sisi ni. . .Hu—huna budi kujihurumia mwenyewe, kwa sababu hujakubali njia iliyowekwa na Mungu ya kuepukia.

⁷² Sasa, Mungu anapoweka njia Zake, sijui tu ni *kwa nini* Yeye hujisikia anapotuwekea njia, kwa ajili ya uponyaji wetu, kwa ajili ya wokovu wetu, kwa ajili ya faraja yetu, kwa ajili ya amani yetu, na mambo haya yote, nasi tunaondoka tu na kuziacha. Hapana shaka tunamfanya ajisikie vibaya sana.

⁷³ Kwa hiyo wakati mmoja katika Biblia, katika Kitabu cha Wafalme wa Pili, kulikuwa na m—mfalme aliyekuwa mfalme wa—wa Yuda, naye, jina lake lilikuwa ni Ahazia, alikuwa mwana wa Ahabu na Yezebeli. Alikuwa halifa wa baba yake Ahabu kwenye kiti cha enzi, baada ya Ahabu, yule mwamini mkwamia mpakani, mwasi wa Injili, mshiriki vuguvugu wa kanisa, alienda kule na kumwoa msichana mpagani ili kuimarisha ufalme wake, akaingiza ibada za sanamu katika Israeli wakati huo. Loo, ni jambo la kuchukiza jinsi gani alilofanya!

⁷⁴ Ndipo maskini mke wake mpagani akayachukua maisha ya Nabothi wa thamani kusudi mfalme apate kuchukua urithi wake. Ndipo nabii huyo akatabiri yale yatakayompata, na yale yangempata mkewe, mbwa wangemla barabarani, na wangeiramba damu ya Ahabu kutoka kwenye gari lake la farasi. Na hivyo ndivyo ilivyotukia hasa.

⁷⁵ Ninaweza kuwazia wakati ambapo Yehoshafati, mtu wa Mungu, wakati kweli hakupaswa ku—kushirikiana na kundi baya. Mwaminio hana ushirika na asiyeamini.

⁷⁶ Kunguru na hua hawawezi kuongea pamoja. Kunguru hula mzoga wa kale, uliokufa, hua ni ndege mmoja asiye na nyongo, kama angeula huo mzoga uliokufa, ungemwua. Ni ndege aliyeumbwa maalum, ndivyo hua a—alivyo. Hua hula nafaka pekee, hana nyongo, asingeweza kuimeng'anya. Vivyo hivyo na Mkristo, hawana nyongo ya uchungu ndani yao, hawawezi kula mambo ya ulimwengu. Kunguru angeweza kula hivyo vitu, ngano, na pia anaweza kula mzoga, yeye ni mnafiki.

⁷⁷ Naye hua, ninataka kuwaambia jambo fulani, hua si lazima atafute maji ya kuoga. Je, mliwahi kumchukua hua mdogo, ukasugulia mkono wako juu yake? Amejaa mafuta. Kuna kitu kinachotoka ndani kuja nje na kumdumisha kuwa safi. Loo, jamani! Mwili wake unatiwa mafuta, kutokana na mafuta yanayotoka mle ndani. Amina. Sitaki kuanza juu ya hilo, nitaondoka kwenye somo langu. Lakini yeye hudumisha mwili wake, manyoya yake, mavazi yake safi kwa mafuta yaliyo ndani. Kila wakati anapoufanyisha kazi mwili wake, hiyo hutenda kazi

kule juu kwenye manyoya yake na kumdumisha safi daima, wakati wote. Loo, Damu ya Yesu Kristo humtakasa mwaminio mchana na usiku!

⁷⁸ Ndipo Ahabu akashuka akaenda, na akafanya ushirika na Yehoshafati, ama, Yehoshafati na Ahabu. Naye. . .

⁷⁹ Kila unapowaona baadhi ya walimwengu wasioamini, “Je, waweza kuja kwenye karamu yetu ndogo ya kadi, mpenzi?” kuwa mwangalifu.

⁸⁰ “Vema, unajua unafanya kazi hapa naye bosi wako anakutaka. . . tutakuwa tu na mambo machache ya kijamii usiku wa leo.” Kaa mbali nalo, liondokee.

⁸¹ “Vema, ni Krismasi, una haki ya kuwa na maskini burudani safi.” Usiamini hilo, kaa mbali nalo, jiepushe na kila uovu, usiukaribie.

⁸² Lakini Yehoshafati akawa dhaifu, akashuka kwenda kumwona Ahabu. Naye Ahabu alikuwa na kusudi fulani, akasema, “Vema, tuna ardhi fulani hapa juu, ni mali yetu.” Akamwonyesha mambo yote makuu. Na hivyo ndivyo ibilisi afanyavyo, kuwaonyesha mambo yote makuu aliyo nayo, mnaona, yote aliyo nayo. Vema, kule kumetameta, hiyo dhahabu, kwa namna fulani iliyaangaza macho yake, mwajua, naye akawazia, “Jamani!” Haikuyaangaza, iliyapumbaza.

Na kwa hiyo hatimaye wakaketi huko nje, naye akasema, “Vema, twende Ramoth-gileadi, ama nita- . . . -vuta?”

Akasema, “Inatupasa kumtaka shauri Bwana juu ya jambo hili.”

⁸³ Kwa hiyo Ahabu akasema, “Loo, bila shaka! Um-hum. Tunapaswa kufanya hivyo. Nina mfumo bora zaidi wa kikanisa uliopo nchini.” Anashuka kwenye seminari yake na kuwatoa manabii mia nne. Hiyo ni kweli. Wamevalia nadhifu, na ukosi uliopinduliwa, na loo, walikuwa ni watu wazuri sana, kila mmoja wao ni wa kikanisa, wanatheolojia hodari sana.

⁸⁴ Kasema, “Vema, waungwana, mmelishwa vizuri na kutunzwa, lakini jambo hili kuu, sasa, ninawaambia kile ninachotaka mfanye: Nitabirieni mniambie kama inatupasa kwenda Ramoth-gileadi. Hivi mnaona jinsi majoho yangu yalivyo makubwa, na jinsi nilivyo askofu mkuu? Na huyu hapa pia Askofu *Nanii* kutoka hapa juu kwenye ule ufalme mwingine. Tutaunganisha majeshi pamoja. Mwajua, tutakuwa tumeungana basi, kwa hiyo tutafanya mambo makuu, mwajua.”

⁸⁵ Kwa hiyo mmoja wao hata alijitengenezea jozi ya pembe, na kuanza kukimbilia katikati ya kusanyiko akisema alikuwa akiwasukumia nyuma Washami wote. “Nchi yote ni mali yetu, na kwa hiyo mtashinda kwa hizi.”

⁸⁶ Mwajua, kuna jambo fulani kuhusu mwaminio, kama aliwahi kukutana na Kristo kamwe hawezi kuambatana na

upuuzi wa namna hiyo. Hata hivyo, maskini Yehoshafati aliyeketi pale, alisema, “Hivi hakuna mmoja tu zaidi?”

⁸⁷ “Ati mmoja zaidi? Mbona, hawa hapa watu mia nne walioelimika sana, walio bora kuliko wote nchini, nao ni manabii. Kwa nini tuulize mmoja zaidi? Kila mmoja wao ana D.L.D., Ph.D., L. maradufu, Q.S.T. Mbona, wao ni... Jamani, usingeweza kuomba digrii zaidi! Jamani, wanajua Maandiko ndani na nje, nyuma, na mbele.”

Yehoshafati akasema, “Lakini unajua, nina hisia kidogo ya kigeni. Laiti tungalikuwa tu na... Hivi hakuna mmoja tu zaidi?”

“Loo,” akasema, “naam, lakini yeye ni mtakatifu anayejibingirisha, na jina lake ni Mikaya, mwana wa Imla, lakini,” kasema, “Ninamchukia.” Loo!

Kwa hiyo Yehoshafati akawazia, “*Hayo—hayo yanasikika kama ni tikiti ya posho.*” Kwa hiyo, “Mfalme asiseme hivyo. Lakini ningependa kusikia yale asemayo.”

⁸⁸ Kwa hiyo mkimbiaji mmoja akakimbia kule kwenye kibanda kidogo alimokuwa, lile kusanyiko dogo mahali fulani pale pembeni, mwajua, naye akasema, “Loo, Mikaya, unajua nini? Lazima... Sina budi kutia kinasa mazungumzo sikioni mwako sasa.” Mnaona? “Wewe sema jambo lile lile wanalosema. Useme tu kama wasemavyo, kwa sababu nakwambia, kwamba wahudumu wote mia nne wanasema tunapaswa—tunapaswa kufanya *hivi*, kwa hiyo huna budi kusema jambo lile lile.”

⁸⁹ Mikaya akasema, “Kama Bwana Mungu aishivyo, nitasema tu yale atakayoweka kinywani mwangu.” Ninapenda hilo, ninapenda hilo. Um-hum.

⁹⁰ Kwa hiyo wakamleta kule chini, Ahabu alikuwa na kipindi cha hasira kali, “Mleteni huyo mtakatifu anayejibingirisha miongoni mwetu hapa chini, italiangamiza kusanyiko letu hakika kabisa.” Kwa hiyo basi, muda si muda mwajua wakati alipokuja, alisema, “Sasa, ninakuonya, hatasema chochote ila uovu juu yangu, maana ninajua yeye daima ananichimba kuhusu wanawake wangu kukata nywele zao, na mambo haya yote. Loo, yeye ni mtakatifu anayejibingirisha, kweli!”

Sasa, yeye akasema, “Hata hivyo nitadumu moja kwa moja na Neno.”

Kwa hiyo akasema, “Mikaya, niende Ramoth-gileadi nikachukue mali yangu, au niache?”

Kasema, “Nipe usiku wa leo, hebu nione yale Bwana atakayosema.”

Kwa hiyo baada ya huo usiku kupita, akarudi. Kasema, “Unasemaje?”

Kasema, “Kwea, ukitaka.”

Akasema, “Nitakuapisha hata lini,” alijua kulikuwa na kasoro katika hilo, “kwamba uniambie tu ukweli.”

Kasema, “Kwea,” akasema, “lakini niliwaona Israeli kama kondoo waliotawanyika bila mchungaji.” Naye akasema...

⁹¹ Kwa nini? Alikuwa akidumu na Neno la Mungu. Alikuwa akisema jambo lile lile Neno lililosema, kwa sababu Neno la Mungu lilikuwa pamoja na nabii. Naye nabii Eliya alisema asingeweza kutabiri mema dhidi ya mtu aliyekuwa mwovu kama Ahabu. Kwa hiyo nabii, Neno lilikuwa tayari limesema ya kwamba Ahabu atauawa, Yezebeli atalishwa kwa mbwa. Na kwa hiyo, Mikaya angeweza kusema nini tofauti na yale Neno liliyosema? Kweli, ilimbidi kudumu na Neno. Haidhuru linasikika kubwa jinsi gani na jinsi linavyosikika kuu, liangalieni Neno, Hilo daima ndilo kweli.

⁹² Na kwa hiyo, huyu mzee mashuhuri wa jimbo, ama askofu, chochote kile, akajasiria kumpiga kofi mdomoni, na kusema, “Neno la Mungu lilitokaje kwangu, kama lilienda kwako?”

⁹³ Akasema, “Utaona siku moja.” Akasema, “Nilimwona Mungu ameketi kwenye kiti cha enzi, na jeshi lote la Mbinguni lilikuwa limemzunguka, Naye akasema, ‘Ni nani tunayeweza kumfanya ashuke aende akamdanganye Ahabu apate kumpeleka huko nje na kuufanya unabii wa Eliya kutimia?’” Mungu huangalia hilo, mwajua. Kasema, “Ningemtuma nani kwenda huko nje?”

⁹⁴ “Ndipo pepo wa uongo akapaa kutoka chini, labda kuzimuni, akaja na kusimama mbele Zake, kasema, ‘Nitashuka niende niingie ndani ya hao wahubiri na kumfanya kila mmoja wao kutabiri uongo.’”

⁹⁵ Neno la Mungu litatimizwa, ndugu, sijali kinachotukia. Yohana alisema, “Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto.” Neno la Mungu!

⁹⁶ Mwana wa mtu huyo alikuwa amechukua kiti chake cha enzi baada ya kifo chake. Siku moja akitembea huko nje, bado alikuwa amewachukia hao manabii, naye akatembea huko nje siku moja dirishani mwake na alikuwa akiangalia pande zote, ndipo akaanguka kupitia dirishani akaumia, Biblia ilisema alikuwa mgonjwa. Kwa hiyo akawaita baadhi ya watu wake na kutuma wawili wao, ama kundi dogo la askari, huko Ekroni, kwenda kuwataka shauri manabii wa Baalimu, kama angepona au la.

⁹⁷ Kwa hiyo, mwajua, Mungu huwajulisha manabii Wake siri Zake. Hiyo ni kweli? Kwa hiyo, Eliya kule chini mlimani, huko nyuma pangoni, amelala juu ya lundo la—lundo la kichaka, ama chochote kile, huko nyuma, amejifunika koti lake, Bwana akasema naye. Basi akaenda kule na kusimama barabarani, Yeye akasema, “Panda uende kule. Simama pale, kwa sababu wanapanda juu.”

⁹⁸ Loo, askari hawa wakapitia pembeni, wakaangalia, huyu hapa maskini mhubiri mwembamba aliyejaa nywele anakuja akitembea barabarani, ndevu zimejaa usoni mwake, amejifunga kipande kikubwa cha ngozi, hakuonekana mtu wa kuvutia sana, bali alikuwa na BWANA ASEMA HIVI, hilo ndilo jambo muhimu. Hakuwa *mwungwana* sana.

⁹⁹ Kwa hiyo, akawasimamisha, akasema, “Kwa nini mnaenda huko Ekroni?” Kasema, “Nendeni mkamwambie, ‘Mbona akatuma ujumbe kule? Je, ni kwa sababu hakuna Mungu katika Israeli? Huku hakuna nabii wa kumtaka shauri? Kama alitaka kujua jambo fulani kulihusu, mbona hakumwuliza Mungu? Anadhaniwa kuwa mfalme hapa, wa Israeli, kwa hiyo kwa nini hakumwomba Mungu? Ni kwa sababu hatuna Mungu hapa? Ni kwa sababu hatuna na—nabii hapa chini?’ Lakini kwa sababu amefanya jambo hili, nendeni mkamwambie, ‘BWANA ASEMA HIVI, hatoki kwenye kitanda hicho.’” Loo, jamani!

¹⁰⁰ Nashangaa leo, kwa nini wanaume wanataka kuvuta sigara? Kwa nini watu wanataka kukaa nyumbani Jumatano usiku, kuangalia kipindi cha televisheni, badala ya kwenda kwenye mkutano wa maombi? Ni kwa nini tunataka kufanya hivyo? Kwa sababu hakuna furaha katika nyumba ya Bwana? Ni kitu gani kinachomfanya mtu atake ku—kunywa pombe, na kukimbia huku na huku, na kutenda namna hiyo? Je, ni kwa sababu hatuna Mungu yeyote? Je, ni kwa sababu hakuna furaha katika nyumba ya Bwana, tena? Je, ni kwa sababu Roho Mtakatifu hayuko tayari kutubariki sisi sote? Ana—ana kasoro yoyote?

¹⁰¹ Lakini kwa sababu tunafanya hivyo, hiyo ndiyo sababu tumelaaniwa, hiyo ndiyo sababu Mungu ameweka kitu hiki juu ya kanisa, baridi hii na unyevu, tunaenda mahali pengine tupate raha, badala ya kuja nyumbani mwa Bwana tupate raha. Nyumba ya Bwana ni furaha ya Bwana, furaha ya Bwana ni furaha ya watu Wake. Anakutaka uje kanisani na kumwabudia, na uwe na furaha, na kuridhika, ukimpa Mungu sifa, na heshima, na utukufu, na hekima, na nguvu, na mamlaka, Yeye anakutaka ufanye hivyo.

¹⁰² Na sasa, mnajua wakati wajumbe hawa waliporudi, na kwa hiyo wakaona . . . wakaingia kwa mfalme huyu, nao wakasema, “Mtu fulani alitumbia turudi, na kutwambia *hiki-na-hiki*.”

Akasema, “Alikuwa ni nani? Alikuwa amevaa nini?”

Kasema, “Alikuwa amejaa nywele, na alikuwa na kipande cha ngozi kiunoni mwake.”

Naye akasema, “Huyo alikuwa, Eliya, nabii wa Mungu, yule Mtishbi.”

¹⁰³ Loo, jamani! Alijua yaliyokuwa yanakuja. Haikuwa kwa sababu hawakuwa na Mungu, haikuwa kwa sababu hawakuwa na nabii, bali ilikuwa—ilikuwa ni njia za kijinga za mfalme

mwenyewe, ilikuwa ni matendo yake mwenyewe ya kichoyo na maovu, kama mama na baba yake. Alimchukia nabii huyo.

¹⁰⁴ Hiyo ndiyo sababu siku hizi hukumu imeukalia ulimwengu, sio kwa sababu hatuna Mungu, si kwa sababu hatuna manabii, lakini ni kwa sababu watu wanazichukia njia za Bwana, na kuzipenda njia za ulimwengu. Ni kweli kabisa.

¹⁰⁵ Ni kama tu mwanadamu, mgonjwa, akifa kwenye vipandio vya mlango ya daktari kwa sababu anakataa kunywa dawa yake; jambo lile lile. Anafia kwenye vipandio vya mlango wa daktari akiwa na dawa ya kutosha ndani kwa ajili ya ugonjwa wake, bali anakataa kuinywa. Hilo si kosa la daktari, si kosa la hiyo chanjo ya dawa, ni kosa la mtu huyo, kwa sababu hatadungwa hiyo chanjo. Hivyo tu. Na hilo ni jambo hatari, hakika ni hatari. Huwezi kusema daktari ndiye aliyesababisha hilo, nawe uko moja kwa moja mlango pake, hutainywa dawa yake, na hata hivyo ana kitu fulani.

Sasa, unasema, “Unaamini katika kunywa dawa?”

¹⁰⁶ Ninaamini katika chochote kinachosaidia jamii ya binadamu ni cha kiungu. Bila shaka, ndivyo ilivyo. Ndivyo hasa. Niambieni ni kwa nini tunaninii...tungefanya nini leo bila kliniki hizi na hospitali, na kadhalika? Bila shaka. Najua kuna baadhi zilizofungwa nyuma ya mlango nilipoanza kuondoka, lakini yote hayo yalifika wapi? Mnaona, huna budi kuzingatia chochote kilicho cha busara. Chochote, kama—kama dawa, hospitali si za Mungu, zinampinga Kristo, zitetekezeni, ziondoeni nchini, hakika. Lakini ni kitu cha kuwasaidia, bila shaka.

¹⁰⁷ Lakini hakuna hata moja ya hizo inayoweza kukuponya. Hakuna dawa ulimwenguni, hakuna daktari...kama yuko, yeye ni bingwatapeli, yeye si daktari halisi. Daktari akikwambia ya kwamba wana dawa itakayokuponya, yeye hajui anachozungumzia. Mayo Brothers wanasema hakuna dawa ulimwenguni itakayokuponya, kasema, “Kuna Mponyaji mmoja tu, huyo ni Mungu, tunadai tu kuyasaidia maumbile.”

Kama nilivyowaambia, kama nikiukata mkono wangu, nianguke nife papa hapa, da—dawa zote nchini zisingeweza kuponya mahali hapo palipokatwa na kisu.

Unasema, “La, umekufa.”

¹⁰⁸ Vema, hebu na wauhifadhi mwili wangu kwa dawa, na nionekane ni wa kawaida kwa miaka hamsini tena, na kunidunga penisilini kila siku, na kadhalika, kwa haungepata nafuu hata kidogo, waupake marhamu, na kuushona, na kunipa vyote...haingefaa kitu. Kama imetengenezwa kuuponya mwili, kwa nini isiuponye? Huo hapo umelala.

Mnasema, “Uhai umetoka.”

¹⁰⁹ Hiyo ni kweli. Sasa, uhai ni nini? nami nitawaambia Mungu ni Nani. Ni kweli kabisa. Mungu ndiye Mponyaji. Daktari anaweza kuurudisha mfupa, bali hawezi kuuponya.

¹¹⁰ Vipi kama nilikuwa nikizungusha mpini wa gari langu, nikavunja mkono wangu, kisha nikaingia mbio, kasema, “Aisee Daktari, niponye mkono wangu upesi sana ili niweze kutoka nje, nimalize kuuzungusha mpini wa gari langu. Siwezi kukiwasha kitu hicho?”

Angesema, “Unahitaji uponyaji wa akili.”

¹¹¹ Hiyo ni kweli. Huenda akaurudisha, bali hawezi kuuponya. Hiyo ni kweli. Anaweza kung’oa jino, bali hawezi kuponya tundu lilimotoka. Anaweza kukata kidole tumbo ubavuni mwako, bali hawezi kuponya mahali alipokata, maana hakuna dawa ambazo zitajenga seli, kuzidisha seli.

¹¹² Na kabla hujaweza kuponya chochote, haina budi kuwa ni ongezeko la seli, kwa hiyo Mungu ndiye Mponyaji pekee. Huwezi kulifanya Neno la Mungu likosee, Zaburi 103:3 ilisema, “Mimi ni Bwana, nikuponyaye magonjwa yako *yote*.” Nimehojiwa kwenye Mayo Brothers, na mahali pengi, nao wanasema hivyo. “Sisi si waponyaji, hatudai kuwa waponyaji, tunasaidia tu maumbile. Kuna Mponyaji mmoja, huyo ni Mungu.” Kwa hiyo Mungu ndiye Mponyaji.

¹¹³ Mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, kasema, “Vema, Ndugu Branham, nitakuuliza swali basi.” Kasema, “Vipi kuhusu penisilini kwa mafua?”

¹¹⁴ Nikasema, “Vema, jamani, jamani! Natumaini wewe si mnyonge hivyo.” Nikasema, “Angalia, vipi kama una nyumba iliyojaa panya wanaotoboa mashimo kote kwenye paa, na kadhalika, na huko chini kila mahali kuna wengi, umeweka sumu nyingi sana ya panya na kuwatia hao panya sumu? Inawaua hao panya wote, hiyo haiyazibi hayo mashimo. Penisilini huua tu kijidudu, kiini cha mafua, haijengi tishu iliyoharibu, huwatia tu panya sumu, hivyo tu, Mungu hana budi kuziba hayo mashimo. Hivyo tu. Yeye ni Bwana ayaponyaye magonjwa yetu yote. Naam, bwana.

¹¹⁵ Nami namshukuru Mungu kwa kila chanjo waliyopata, kwa ajili ya chanjo ya Salk, tunaomba daima kwamba Mungu atatupa kitu fulani kwa ajili ya kansa, kwa ajili ya watu maskini wanaoteseka. Chochote kinachoweza kufanywa kusaidia, ninakiunga mkono, naam, bwana, ninakiunga mkono asilimia mia moja. Na kama sisi Wakristo tungeomba zaidi kwa ajili ya mambo kama hayo, tungekuwa bora zaidi, nchi nzima ingekuwa, naam. Watu mashuhuri, wanatoa maisha yao wakijaribu tu kupigana na mambo hayo yanayowalemaza watoto, na kila kitu, bila shaka.

¹¹⁶ Hakika ninamshukuru Mungu kwa yote aliyotufanyia. Ninamshukuru Mungu kwa ajili ya motokaa, ninamshukuru

Mungu kwa ajili ya sabuni ya kunawa mikono yangu, na hiyo mitambo yote, mambo hayo yote, ninamshukuru Mungu kwa ajili yake, bila shaka. Kuna wakati mmoja hatukuwa na sabuni, mwajua, kuna wakati mmoja hatukuwa na motokaa. Kama nilitaka kwenda Phoenix ningeweza kuondoka niende, bali ninamshukuru Mungu kwa ajili ya motokaa, nitaingia ndani yake, nimtumainie moja kwa moja safarini niwezavyo kwenda. Mnaona? Kwa hiyo, tunamshukuru Bwana kwa ajili ya vitu hivyo. Mambo yote ambayo ni mazuri kutusaidia yanatoka kwa Mungu, bila shaka.

¹¹⁷ Lakini sasa, vipi kama huyo mgonjwa ameketi huko nje kwenye vipandio vya daktari na anakataa tu kunywa dawa yake? Basi huyo mgonjwa akifa, si kosa la hiyo dawa.

¹¹⁸ “Je, hapana zeri katika Gileadi? Huko hakuna tabibu? Basi kwa nini haijarejea afya ya binti Yangu, watu Wangu? Kuna kasoro fulani?”

¹¹⁹ Ni jambo lile lile kanisani. Wanaume na wanawake huketi kanisani na kufa katika dhambi zao, kwa sababu wanakataa zeri ya Mungu. Hiyo ni kweli. Si kwa sababu hakuna zeri hapa, Roho Mtakatifu yupo hapa, tuna madaktari wengi, matabibu. Kwa hiyo watu hufa katika dhambi zao, usimlaumu Mungu, kuna zeri katika Gileadi, na kuna matabibu huko, lakini ni mtazamo wa watu juu yake.

¹²⁰ Sasa, kama u—ukinywa kitu kama dawa, ni jambo baya sana kama ungekataa dawa. Ni jambo la kuchukiza zaidi jinsi gani kama ukikataa zeri ya Mungu kwa ajili ya nafsi yako, ukiikataa dawa hiyo, basi itakuwaje? Umepotea milele kama ukiikataa hiyo. Loo, wewe, mwili wako huenda ukaukarabati vilivyo.

¹²¹ Halafu jambo lingine, unaweza kunywa dawa, iliyo nzuri kwa mmoja, itamsaidia mmoja, itamwua mwingine. Penisilini karibu huua theluthi moja ya wale inaowasaidia, itawaua wengine na kuwasaidia wengine, ni kitu hatari sana. Basi kile kitakachomsaidia mmoja, kitamsaidia huyo mwingine. Lakini si lazima uhofie kuhusu dawa ya Mungu, inasaidia, “Kila atakaye, na aje.” Naam, bwana. Ni kwa ajili ya wote, huna haja ya kuhofu juu yake, hakuna hatari ya kujipumbaza nayo.

¹²² Ukianza kujipumbaza nayo, unasema, “Vema, nakwambia, Ndugu Branham, si—siamini ni kwa ajili yangu.” Kama vile watu wasemavyo siku hizi, “Kamwe siwezi kujizuia kuvuta sigara. Kamwe siwezi kujizuia kuzurura.”

¹²³ Mtu mmoja aliniambia si muda mrefu uliopita, akasema, “Nina mke mzuri, lakini, Ndugu Branham, sikuumbiwa mwanamke mmoja.” Kasema “I—inanibidi kuzurura na wanawake wengine.”

Nikasema, “Unajua una shida gani? Unakataa tu tiba.” Hivyo tu.

¹²⁴ Hiyo ndiyo shida ya watu siku hizi. Sababu ya wewe kunywa pombe, kuvuta sigara, kusema uongo, kuiba, na kuzozana, kufanya yasiyofaa, unakataa zeri ya Mungu ya upendo inayotuleta pamoja na kutufanya kitu kimoja. Si kwa sababu hakuna nguvu za kutosha za Mungu hapa kutuma uamsho kote mjini, tunakataa tu kuzitumia, hivyo tu. Amina. Zi—zi—ziko hapa, bali kama ukifa katika dhambi zako, kutokuamini kwako, si kosa la Mungu, si kosa la Roho Mtakatifu, si kosa la kanisa, kwa sababu tu watu wanazikataa.

¹²⁵ Wanasema ugonjwa wa moyo ndio mwuaji namba moja. La, la, shida ya dhambi ndiyo mwuaji namba moja, hiyo ni kweli, mwuaji namba moja. Imeingia katika makundi yetu ya Kipentekoste.

¹²⁶ Mtu fulani alikuwa akizungumza nami leo kuhusu Wapentekoste, naye akasema, “Unajua nini, Ndugu Branham, inakuwa tu kama sijui-nini.” Kasema, “Unajua watu wetu wengi walivyo, wana watoto wao, wanawaingiza moja kwa moja ndani, wanawaweka kwenye kitanda cha watoto wachanga, nao wanakua, na hivyo ndivyo, wanatarajia tu iwe hivyo.”

¹²⁷ Kama vile David duPlessis alivyosema wakati mmoja kuhusu kitu kama hicho, “Mbona, huwezi kuingia namna hiyo. Hilo ndilo—hilo ndilo lililowafanya Wamethodisti kuwa jinsi walivyo, hilo ndilo lililowafanya Wabaptisti kuwa jinsi walivyokuwa. Waliendelea tu kuwaingiza watoto wao, wakawaweka kwenye kitanda cha watoto, na kuwalea. Mungu hana wajukuu wowote, Yeye anao tu wana, wana na binti, si wajukuu wa kiume na wa kike, Mungu hana wajukuu. Yeye si, unajua, Mungu—Mungu si Babu, Yeye ni Baba.” Amina.

¹²⁸ Natumaini siwaudhi, bali natumaini nitawatisha kidogo, hata hivyo, kuanzisha jambo fulani. Mungu hana wajukuu. Na wakati wewe...kwa sababu tu ati ulikuwa Mpentekoste, baba yako na mama yako waliilipa gharama, hilo halikufanyi Mpentekoste mpaka ulipe gharama ile ile, na upate kitu kile kile walicho nacho. Naam, bwana. Kuna nyingi sana iliyosalia, bado kuna zeri nyingi huko Gileadi, dawa nyingi sana kule kwa ajili ya dhambi, kutokuamini. Naam, bwana.

¹²⁹ Ndugu zetu wa Kipentekoste wakisimama, wakisema, wakikana uponyaji wa Kiungu, na mambo kama hayo, ni kwa sababu tu unaikataa dawa, ewe mjukuu. Si mwana wa Mungu, mwana wa Mungu anazaliwa kwa Roho wa Mungu, yeye ni mtoto wa Mungu. Lakini Mungu hana wajukuu wowote. Kweli.

¹³⁰ Mnajua kuna nini? Wanaogopa kuzaliwa upya, hiyo ndiyo shida yenyewe. Hebu nikwambie jambo fulani, ndugu, sijali ni kuzaliwa kwa namna gani, kuzaliwa kokote ni machafuko. Kama kuko kwenye zizi la nguruwe, ama kama kuko zizini, ama kama kuko kwenye chumba cha hospitali cha waridi, kilichopambwa, kuzaliwa kokote ni machafuko. Nako kuzaliwa

upya ni vile vile, kutakufanya ushuke chini na kulia vikali, na kwa sauti kuu, na kufanya mambo ambayo kamwe hukuwazia ungefanya hapo awali, moja kwa moja huko chini, ambako, ndugu, ninamaanisha yataleta Uzima mpya, hakika kabisa.

¹³¹ Huenda kukavuruga theolojia yako, huenda kukavuruga karamu zako za kadi huenda kukavuruga kuogelea kwako, na kucheza dansi, na kuteleza kwenye theluji, huenda kukakufanya ukate nywele zako, huenda kukakufanya upate kitu tofauti, na kukufanya uache kuvuta sigara, ni mchafuko, bali huleta Uzima. Amina. Kile tunachopaswa kuwa nacho ni kuzaliwa, Uzima, ni machafuko, hayana budi kuchafuka kabla hayajawa sawa. Naam, bwana. Huna budi kuwa na: “Chembe ya ngano isipoanguka ardhini na kuoza,” machafuko, unajichafua nayo, hiyo ni kweli, unakufa tu. Ushuke uende kule, na . . .

¹³² Mwanamke mmoja aliniambia wakati mmoja, kasema, “Loo, ningeona aibu! Hao watu huko chini,” kasema, “nisingeweza hata kukusikia ukihubiri,” kasema, “mbona, hao wanawake na wanaume wikipiga mayowe, ‘Haleluya! Amina! Bwana asifiwe! Nisingeweza kusikia ulichokuwa unasema.”

Nikasema, “Kama hawakusema hivyo, ingeniogopesha hata kufa.”

Akasema, “Wakati mwanamke huyo aliposimama kule nyuma na kuanza kulia,” kasema, “mzizimo tu uliingia mgongoni mwangu.”

¹³³ Nikasema, “Kama ungefika Mbinguni, ungeganda hata kufa,” nikasema, “kwa sababu kila mtu atakuwa akipiga mayowe, na kupaza sauti, na kumsifu Bwana Mungu wetu, Mungu mmoja na wa pekee.” Sawa.

¹³⁴ Wanaogopa nini? Kuzaliwa upya. Hiyo ndiyo sababu tuna wajukuu kanisani. Tunaogopa kuzaliwa upya, tunamwogopa Roho Mtakatifu, tunaziogopa nguvu za Mungu, wanaogopa zita—wanaogopa zitawafanya waoshe baadhi ya vipodozi kutoka kwako, ama chochote kile, hiyo ndiyo shida. Mungu tutumie uamsho wa kale . . . ? . . . kumleta Roho Mtakatifu tena, Yuko kwa wingi.

“Je, hakuna zeri katika Gileadi? Huko hakuna matabibu?”

Hakika, kuna matabibu hapa, zeri nyingi hapa, pia.

“Basi mbona haijarejea afya ya binti ya watu Wangu?”

¹³⁵ Ni kwa sababu watu wanaikataa. Amina. Jambo ndilo hilo. Wanakataa kukusanyika pamoja, wanakataa kufanya uamsho. Hiyo ndiyo shida, ubinafsi, na kadhalika ulichukua mamlaka. Kuna zeri nyingi huko Gileadi, kuna matabibu hapa, lakini watu wanaikataa, hiyo ndiyo shida.

¹³⁶ Kuna wakati ambapo hatukuwa na dawa ya homa ya matumbo, wakati ambapo hatukuwa na dawa ya chanjo ya—ya—ya Salk, na vitu kama hivyo, na, lakini sasa tunayo. Hiyo

ni kweli kabisa, tunayo sasa, Mungu ashukuriwe kwa ajili yake. Kulikuwa na wakati ambapo dawa yetu ya wokovu haikuwa nzuri sana, maana ilikuwa ni wana-kondoo, na kadhalika, na mbuzi, lakini sasa dawa imebadilishwa. Bila shaka.

¹³⁷ Wakati... Kwa nini wanapata tiba kwa ajili ya dawa? Unajua wanafanya nini? Wanachunguza, wanaweka *kiasi fulani* cha—cha *hiki* ndani, na *kiasi fulani* cha *hiki* ndani, dawa ya kutosha ku—ku—kuua sumu, na *kiasi fulani*, na kuchunguza hali ya mgonjwa, na jinsi ninii yake ilivyo na nguvu... Kamwe usinywe dawa pasipo kumwuliza daktari halisi kuihusu, maana inaweza kukuua. Na kwa hiyo basi, kwa hiyo wao—wao wanaona.

¹³⁸ Ndipo basi, muda si muda mwajua, wanamdunga maskini nungubandia, kama akinusurika nayo, basi wanakupa wewe. Na wakati mwingine... Miili yote ya binadamu haijafanywa kama nungubandia, mwajua, hiyo ndiyo sababu inawaua baadhi ya wanadamu. Mnaona? Wanamfanyia majaribio maskini nungubandia, na kama jamaa huyo mdogo akipona, basi wanakupa wewe. Vema, hivyo ndivyo wanavyoijaribu dawa, mnajua hiyo ni kweli. Wanachukua kitu fulani na kumpa huyo nungubandia, na kama akinusurika nayo, basi wanakupa wewe, hiyo ndiyo sababu wanaua wagonjwa wengi sana, kwa sababu sisi sote hatujafanywa kama nungubandia.

¹³⁹ Vema, hebu niwaambie jambo fulani, wakati Mungu alipojaribu Dawa Yake, kamwe hakumchukua nungubandia, alijitoa Mwenyewe. Ee Mungu! Wakati alipobatizwa kule na Yohana kwenye kingo za Yordani, ndipo ile chanjo ikashuka kutoka Mbinguni, “Huyu ni Mwanangu mpendwa ninayependezwa kukaa ndani Yake,” waliangalia, waone kama ingeshikilia.

¹⁴⁰ Walipomtemea mate usoni Mwake, ilishikilia vizuri; Yeye, alipotukanwa, hakutukana pia; alipokufa pale Kalvari, aliwaombea adui Zake. Ilishikilia pale Kalvari, ilishikilia katika mauti, ilishikilia duniani, ilishikilia kila mahali. Walimweka kaburini, na kwenye asubuhi ya Pasaka ikashikilia tena. Amina.

¹⁴¹ Nanii, si nungubandia, bali Mwana wa Mungu alikunywa hiyo Dawa, Yeye aliinywa Mwenyewe. Amina. Sasa, sishikwi na msisimko, ninaanza kujisikia kubarikiwa. Naam, bwana. Ni nani aliyekunywa hiyo Dawa? Ni nani aliyejaribu? Loo, haleluya! Yeye Ndiye aliyezichukua dhambi zetu na kuyabeba magonjwa yetu. Aliiweka Dawa juu yake Mwenyewe, si juu ya nungubandia, nabii, ama *kitu kingine*, aliweka juu yake Mwenyewe. Haleluya! Naam, bwana. “*Alijeruhiwa* kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona.”

¹⁴² Ilishikilia katika saa ya kufa, ilishikilia msalabani, ilishikilia katika Gethsemane, ilishikilia chini ya kila majaribu,

chochote kile, hiyo dawa ilishikilia. Amina. Mungu alikuwa akitaka kuujaribu Uzima wa Milele, Naye akauweka katika mwili wa kibinadamu wa Mwanawe Mwenyewe, akaingia na kukaa ndani Yake, ndipo hiyo dawa ikashikilia. Alipofufuka kwenye asubuhi ya Pasaka alivunja kamba za mauti, kuzimu, na kaburi kisha akafufuka.

...akawatokea wale kumi na mmoja walipokuwa wakila, akawakemea kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao na kutokuamini kwao, kwa sababu hawakuwasadiki wale waliomwona akiisha kufufuka katika wafu. (Amina.)

¹⁴³ Kasema, “Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini atahukumiwa. Kwa kuwa nitawapa dawa. Kama nikiwapa dawa hii mambo nifanyayo Mimi, wao watayafanya pia. Nitalichanja Kanisa lote hapa,” Yeye alisema. “Ulimwenguni kote, ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Haleluya! “Ishara hizi nilizofanya, watazifanya pia, maana nitalichanja Kanisa kwa dawa ile ile. Je, mnaweza kubatizwa, dawa ile ile niliyochanjwa?” Amina.

¹⁴⁴ Hiyo ndiyo shida siku hizi, tulichukua baadhi ya kanuni za kale za kanisa badala ya chanjo, hiyo ndiyo sababu dhambi ilipenya ndani. Kama tukimpata Roho yeye yule aliyekuwa juu Yake, ubatizo ule ule, nguvu zile zile, utukufu ule ule, Roho Mtakatifu yeye yule, Atatuchanja kama tu alivyomchanja Yeye, aondoe hofu yote. Haleluya! Kusimama mbele ya adui na kuliita Neno la Mungu Kweli. Amina. Akupe uti wa mgongo kama gogo la msumeno, atoe mfupa wa shingo ya kuku, na kuweka uti wa mgongo halisi ndani yake. Naam, atakuwa hivyo. “Je, mnaweza kubatizwa kwa chanjo niliyochanjwa?”

¹⁴⁵ Hakika ilishikilia maishani Mwake. Wakati alipomtemea mate usoni Mwake, Yeye hakusema, “Enyi maskini wa Utatu, enyi maskini wa Umoja!”

¹⁴⁶ La, la, haikuwa hivyo, la, la, Yeye alikuwa amechanjwa na upendo wa Mungu. “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, kila amwaminiye hatapotea.” Alichanjwa, mwili mdogo, uliozaliwa na bikira alimoishi Mungu wa Mbinguni. Alikuwa amechanjwa na Mungu, Uzima wa Milele ulikuwa ndio chanjo Yake. Nayo ilishikilia wakati wa majaribu, ikashikilia katika wakati wa, wakati kila mtu alipomwacha, ilishikilia, ilidumu vizuri. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁴⁷ ...adui mbele ya mauti. Nao walitaka chanjo iyo hiyo, kwa sababu baada ya kufa na kukaa kaburini siku tatu mchana na usiku, wakati mbingu zote zilipoingia giza, dunia ilishikwa na mavune ya fadhaa, na mi—miamba yote ikakatwa kutoka milimani, na kila kitu kilishuhudia ya kwamba alikuwa amekufa

na alikuwa kaburini, ndipo Jumapili asubuhi hiyo chanjo ikashikilia, kwa sababu Yeye alisema, “Nina uwezo wa kuutoa uhai Wangu, na uwezo wa kuufufua tena. Chanjo hii niliyo nayo itautoa uhai na kuulaza chini, nami nitauinua tena.”

“Ndugu, hilo ndilo ninalotaka. Ninataka kunyosha mkono wangu.”

¹⁴⁸ Huchanjwi mkononi, unachanjwa moyoni. Unyoshe upate chanjo ya ufufuo, wa nguvu za Yesu Kristo. Haleluya! Chanjo. Sasa, hutaki kuandika kanuni yoyote ya imani juu *hapa*, acha tu Kristo aingie, hiyo ndiyo chanjo, kamwe hakuijaribu kwa kanuni ya imani, alijaribu kwa Roho Wake.

“Je, hakuna zeri katika Gileadi? Huko hakuna matabibu?”

Loo, naam, tuna zeri na matabibu pia.

“Basi kwa nini?”

Hiyo ni kusema, Mungu atatuuliza, “Kwa nini?” baadhi ya siku hizi. “Kwa nini?”

¹⁴⁹ Walitaka kuchanjwa, kwa hiyo Yeye akasema, “Nawaambia mtakalofanya, nendeni kwenye mji wa Yerusalemu, kisha mpande kwenye chumba kile cha juu, na mkae humo mpaka chanjo yenu itakapokuja.” Loo, ndugu! “Kaeni mpaka mtakapochanjwa, mpaka dawa itakaposhuka, ile zeri itakaposhuka.”

¹⁵⁰ Basi wote walipokuwa wameketi pamoja, wakiimba nyimbo kwa moyo mmoja, mara ikaja sauti kutoka Mbinguni kama upepo wa nguvu ukienda kasi, ukawachanja watu mia moja na ishirini huko nje. Jamani, ni mpagao jinsi gani wa kukimbia waliokuwa nao! Loo, jamani!

¹⁵¹ Ni kama kumpiga ndama chapa, nilikuwa nikiwapiga ndama chapa, sikuzote nilimhurumia jamaa mdogo. Nami ilinibidi—ilinibidi kuendesha gari nilete hiyo chuma, nanyi Watexas mnajua ninachozungumzia. Na kwa hiyo, wangemfunga miguu minne, na kunyakua maskini chuma hiki pale, na kumchapa kwacho, namaanisha angeshikwa na kifafa. Angerusha mateke, na kulia kwa maumivu, na kuendelea kule kwa muda mrefu, lakini, ewe ndugu, alijua mahali alipotoka tangu hapo na kuendelea, alikuwa amepigwa chapa. Hiyo ni kweli.

¹⁵² Na wakati mwingine itakufanya utende kana kwamba huna akili timamu, bali umetiwa chapa, unajua mahali ulipo, nawe ni mmojawapo wa waliojazwa na Roho Mtakatifu, waliochanjwa.

¹⁵³ Mia na ishirini walichanjwa. Loo, walikuwa na wakati mzuri, kile ninachomaanisha kusema. Kwa kweli walikuwa na wakati mzuri sana. Walitoka humo wote wamechanjwa, walikuwa na Uzima wa Milele, wakijua ya kwamba Mungu angewafufua katika siku za mwisho, nao walikuwa na wakati mzuri sana.

154 Nao walikuwa wamejaa utukufu sana, wengi wao wangeweza kunena katika lugha nne, tano, sita, saba, nane, kumi mbalimbali, bali hata wasingeweza kupata moja ya hizo kutumia kumsifu Yeye, kwa hiyo wao walininii tu, Mungu aliwapa lugha mpya kabisa ya kumsifia, kwa hiyo wakaanza tu kunena kwa lugha zisizojulikana kama Roho alivyowajalia kutamka. Kuwa tu na... Walikuwa wametiwa chanjo. Hiyo ilionyesha walikuwa wametiwa chanjo, walikuwa—walikuwa wakizungumza juu ya Ufalme ambao walikuwa wakiuendea. Walikuwa wametiwa chanjo.

155 Suala la dhambi lilikuwa limekwisha. Isingembidi Petro kutoka nje na kulia kwa uchungu tena, yote yalikuwa yamekwisha basi, alikuwa ametiwa chanjo. Naam, bwana.

156 Nanyi mnajua nini? Baadhi yao hao watu waliona njaa sana kwa ajili ya baadhi ya hiyo, mnajua walifanya nini? Walisema, “Waume na ndugu, tufanye nini? Mna daktari hapa?”

“Naam.”

“Ni nini hii?”

“Hii ni zeri.”

“Mna daktari hapa?”

“Naam, jina lake ni Daktari Simoni Petro.”

“Vema, Petro, utatuandikia maelekezo ya dawa?”

“Naam. Sitaki kuwa nikiandika haya wakati wote, nitaandika tu moja kwa ajili ya wakati wote. Nitawaandikia maelekezo.”

157 Sasa sikiliza, ndugu, unajua nini? Kama maelekezo yameandikwa vizuri, kamwe usiyapeleke kwenye moja ya maduka haya ya bingwatapele ambayo huiwekea kidogo, ama kuongeza kidogo...kutoa kwake. Ukiweka chochote tofauti ndani yake na kuchanganya fomula hiyo, itamwua mgonjwa wako; na ukipunguza kipozasumu kingi kupita kiasi, ama kutia kipozasumu kwa wingi sana humo, haitafaa kitu, kwa hiyo yaache tu jinsi yalivyoandikwa.

158 Akasema... Aina gani ya maelekezo? Yeye alisema, “Tubuni kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea Kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa maelekezo haya ni kwa ajili ya watoto wenu, na watoto wa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Chanjo. Loo, ndugu, tubu na ujipatanishe na Mungu. Ondoa vitu vyote... Mungu aliahidi ya kwamba angekupa Roho Mtakatifu. Hayo ndiyo maelekezo.

159 “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Katika Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya, wakishika nyoka ama kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru, kwa kuwa

wamechanjwa. Nao wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Haleluya! . . . ? . . . Lihubiri jinsi lilivyo.

"Je, hapana zeri katika Gileadi? Au huku hakuna chanjo?"

¹⁶⁰ Kuna chanjo nyingi sana. Haleluya! Whiu! Hmm! Naam, bwana, zeri, zeri katika Gileadi! Kachanjwa. Anaweza kustahimili ladha ya mauti. Aje moja kwa moja mbele ya . . .

¹⁶¹ Mtakatifu Paulo, wakati mmoja walikuwa wakijenga jukwaa la kuikatia shingo yake huko Rumi, nilisimama mahali pale pale, Paulo akasema, "Ee mauti, u wapi uchungu wako? Kaburi, u wapi ushindi wako? Nimechanjwa, utanishikiliaje? Utanijibuje? Lakini Mungu na ashukuriwe, aliyetuma zeri za Gileadi na kuuchanja moyo wangu kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hakuna kitu cha wakati ujao, wakati uliopo, hakuna dhehebu, wala chochote kile kinachoweza kututenganisha na upendo wa Mungu, ulio katika Kristo Yesu." Haleluya! Maadamu tuko ndani ya Mungu, tumechanjwa kutokana na mambo ya ulimwengu.

¹⁶² Mipaka ya kimadhehebu, utairuka moja kwa moja, na kuikumbatia shingo ya ndugu mwingine kama una chanjo. Amina.

Loo, najisikia vizuri. Loo, tulizoea kuimba wimbo mdogo:

Nitaruka niondoke, ee utukufu,

Nitaruka niondoke;

Asubuhi moja angavu wakati maisha haya
yamekwisha,

Nitaruka niondoke.

¹⁶³ Nina furaha sana kuchanjwa. Loo, jinsi Mwana wa Mungu alivyouchukua Uhai Wake Mwenyewe na kuuingiza maishani mwangu, akaingiza maishani mwako, halafu anashuka na kuutia nguvu kwa Uwepo Wake! Loo, jamani!

¹⁶⁴ Unajua, kwa kawaida unapopata chanjo, kila baada ya muda fulani, unachanjwa, bali inakubidi kupata nyongeza, na yale mji huu unayohitaji katika kanisa la Kipentekoste leo ni nyongeza. Haleluya!

¹⁶⁵ Usiiongezee kwa kusema, "Tutaunda madhehebu mengine machache," hilo litaharibu maelekezo yako. Rudi moja kwa moja nyuma na uchukue nyongeza ya kitu kile kile kilichoingia mle kwanza, ubatizo ule ule kwa melekezo yale yale, na Roho Mtakatifu yeye yule. Amina. Amina. Utukufu milele, na milele, utukufu na nguvu katika ufufuo wa Kristo!

¹⁶⁶ Ndipo akasema, "Mambo nifanyayo mimi ninyi nanyi mtayafanya, maana mmechanjwa." Amina. Amechanjwa kwa nguvu za ufufuo, "kionjo cha utukufu wa Kiungu." Amina.

¹⁶⁷ Najua mnafikiri nina kelele, lakini, jamani, ungalijisikia jinsi ninavyojisikia, ungepiga kelele, pia. Nimechanjwa, nimetiwa chapa, nina furaha sana najua mahali nilipo, katika

nyumba ya Mungu. Hivi hamna furaha, enyi Wakristo? Loo, Yeye yupo hapa, loo, bila shaka yoyote. Na tuinamishe vichwa vyetu na kumwabudu.

168 Bwana Yesu, Ee Mungu, Roho Wako ni tajiri sana na:

Jinsi ilivyo tajiri na safi!
Itadumu milele,
Wimbo wa Watakatifu na Malaika.

169 Upendo wa Mungu, unaovuka ng'ambo, unaoingia kwenye vilindi, unaowaendea walioanguka, upendo wa Mungu uliomiminwa mioyoni mwetu na Roho Mtakatifu!

170 Bwana, tuna zeri, tunazo chanjo, tuna matabibu hapa wanaoweza kusoma maelekezo, Mungu, Wewe upo hapa kama Mwuzi dawa kuijaza, na kutoa chanjo. Ninaomba, Mungu, ya kwamba utalijalia kwa kila moyo usiku wa leo usiomjali Kristo. Tujalie. Jalia Roho Wako mkuu ajitokeze sasa na kuonyesha nguvu Zake. Tujalie.

171 Ninapojilaza kwenye hizi lesi, nguo, vitambaa vidogo, jalia Roho Mtakatifu ambaye analeta furaha hii ya chemchemi za Uzima katika kanisa hili, Ee Mungu, jalia aene kupitia kila moja ya vitambaa hivi vidogo. Katika Jina la Yesu Kristo, kila mmoja na abarikiwe, nao watu waponywe. Ninawakabidhi Kwako, Bwana, pamoja na hili kusanyiko, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Amina na amina.

172 Loo, jamani! Jinsi—jinsi nilivyo na furaha! Loo, nina furaha sana, nina furaha sana. Hmm! Nilipokuwa niki-... Nilipokuwa mlinzi wa wanyama pori, nilipitia, kulikuwa na chemchemi ndogo ya kale, ilikuwa ndiyo chemchemi yenye furaha kuliko zote niliyopata kuona, *ilibubujika* tu, *ikabubujika*, *ikabubujika* wakati wote, majira ya kiangazi, majira ya baridi kali.

173 Siku moja niliketi chini kando ya maskini chemchemi hiyo ya kale, nami nikasema, “Mbona una furaha hivi?” Bila shaka asingeweza kunijibu. Nami nikawazia, “Sasa, kama angeweza kunijibu, angesema nini?”

Nikasema, “Una furaha kwa sababu kulungu wanakunywea?”

“La.”

Nikasema, “Unabubujikia nini? Kwa sababu dubu walikunywea?”

“La.”

“Je, unabubujika kwa sababu ninakunywea?”

“La.”

Nikasema, “Ni kitu gani kinachokufanya ububujike wakati wote?”

Kama angeweza kuongea, angesema, “Ndugu Branham, si mimi ninayebubujika, ni kitu fulani nyuma yangu kinachonibubujisha, kinachonisukuma.”

¹⁷⁴ Na hivyo ndivyo ilivyo kwa mwana wa Mungu aliyezaliwa mara ya pili ambaye amechanjwa na nguvu za Yesu Kristo aliyefufuka. “Si Mimi nizatendaye hizo kazi,” alisema Yesu. “Ni Baba anayekaa ndani Yangu, Yeye Ndiye azitendaye hizo kazi.”

¹⁷⁵ Sivyo, endapo kuna mtu hapa asiyelielewa, si watu hawa wanaobubujika, ni *Kitu fulani* humo ndani kinachowabubujisha, hiyo ni kweli, vifoko, chemchemi, zikibubujika. Akamwambia yule mwanamke kisimani, hayo maji yangekuwa chemchemi za maji, zikibubujika katika Uzima wa milele.

¹⁷⁶ Loo, si ajabu yule mshairi alisema, “Ni furaha isiyosemeka na iliyojaa utukufu.” Amina. Whiu! Loo, ninajisikia maradufu ukubwa wangu. Naam, bwana, niko nyumbani sasa. Nina furaha! Nina furaha kwamba tumetoka. Hivi hamna furaha? Loo, jamani, kile Mungu angeweza kufanya na kundi hili dogo sasa hivi!

¹⁷⁷ Yale angaliweza kufanya kama angeweza kamwe kumshika mtu mmoja mikononi Mwake kusudi tu aweze kumshika mtu huyo mmoja! Yeye anaweza—Yeye anaweza kuwafukuza elfu kumi kwa mtu huyo mmoja. Akiwa na mtu mmoja katika imani ya kweli, Yeye anaweza kuwafukuza pepo elfu kumi mbio, upesi wawezavyo kwenda. Naam, bwana. Amina. Nina furaha sana, sivyo?

¹⁷⁸ Tulikuwa tukiimba wimbo mdogo nilipokuja kwa Wapentekoste kwa mara ya kwanza, wangesema, “Nina furaha sana kwamba Yesu aliniweka huru.” Bila shaka, ulikuwa umefungwa kabisa, Yeye akakupa chanjo, hiyo ilitosha, hiyo tu ndiyo iliyohitajika. Amina.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Loo, hilo si linakufanyia jambo fulani? Loo!

Nampenda . . . (Hebu wazia tu jambo hilo.)
Kwani alinipenda kwanza (Alifanya nini?
Alituchanja.)
Na kununua (Kununua Dawa.) wokovu wangu
Mtini Kalvari.

¹⁷⁹ Loo, jinsi nilivyo na furaha! Jinsi nilivyo na furaha kwamba kweli nilipata hii! Jinsi nilivyo na furaha kwamba nimewahi kujua, nimewahi kufikia mahali ambapo ningeweza kutambua kwamba mimi si kitu! Ndipo siku moja akaniinua, akanibusu, akaondolea mbali machozi yangu yote, na kusema, “Wewe ni Wangu sasa.”

¹⁸⁰ Loo, hilo liliuvunja tu moyo wangu, nami nikasema, “Bwana, jalia nitembee pamoja na Bwana katika Nuru ya Neno Lake. Jalia nikae mchana na usiku katika upako wa Roho.” Aibu tu, kwamba inatubidi kuiacha, sivyo? Ni ajabu tu.

¹⁸¹ Kumbukeni, marafiki, ninawapenda. Usiku hautakuwa na giza kupita kiasi, na mvua sana... kunyesha—kunesha sana, pasipo mimi kuwafanyia chochote niwezacho. Kumbukeni tu, mimi ni ndugu yenu, ninawapenda kwa moyo wangu wote.

¹⁸² Kadi zozote za maombi zilizotolewa? Kuna yeyote aliye na kadi ya maombi? Loo, nilisahau. Vema, hakuna haja ya kumwita *mmoja*. Vema, haitubidi kufanya hivyo, Mungu ataponya vivyo hivyo.

¹⁸³ Mnaamini chanjo? Mnaamini ya kwamba Yesu alifanya njia kupitia Damu Yake, kwamba angeweza kuweka chanjo Yake ndani ya mwaminio, naye huyo mwaminio, akiwa na chanjo iyo hiyo ndani yake, itafanya jambo lile lile lililofanya kwa mtu huyo mwingine. Itafanya... Loo, Yeye ni wa ajabu, sivyo? “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya.”

¹⁸⁴ Vema, ninyi watu huko nje, kama Mungu atashuhudia sasa... Ni wangapi walio wagonjwa? Hebu tuone mikono yenu, anayetaka msaada kutoka kwa Mungu, inueni tu mikono yenu. Vema. Loo, hivi Yeye—hivi Yeye si ni furaha tu isiyoneneka na iliyojaa utukufu?

Sasa, hebu na tuwe na kicho tuwezavyo kwa dakika chache, na tumtazamie tu Yeye sasa. Hivi hamninii tu...? Hayo manyunyu ya baraka!

“Tutapata manyunyu ya baraka,”

Uzitume juu yetu, Ee Bwana;

Tujalie sasa kuburudishwa.

Hivi humuupendi huo, kuburudisha huko, Maisha hayo?

¹⁸⁵ Ndugu, dada, nataka kukwambia jambo fulani: Ninawatakeni mnamini ninapozungumza katika Jina la Bwana na kusema, “BWANA ASEMA HIVI.” Kuna Kitu kimoja tu kinachoweza kukuponya, na hicho ni Mungu; na njia moja tu unayoweza kumjia, hiyo ni kwa imani. Hiyo ni kweli?

¹⁸⁶ Sasa, tunajua tunaamini katika kuwekea mikono. Hivi hamwamini hilo? Lakini kama mtanivumilia, daima mmeshangaa, watu husema, “Ndugu Branham, Oral Roberts huwaombea mia tano huku ukiwaombea watano.”

¹⁸⁷ Najua hilo. Hiyo ni kweli. Oral Roberts anawaombea jinsi Mungu alivyomwambia afanye, ninaomba jinsi Mungu anavyoniambia nifanye. Mnaona? Kwa hiyo yeye—yeye—yeye anamtii Mungu, nami ninamtii, pia.

¹⁸⁸ Lakini mnaona, Oral Roberts na ndugu hao kule, wakiwawekea mikono, kama mtanivumilia, hiyo ni desturi ya Kiyahudi, haikuwa hivyo kwa Mataifa.

¹⁸⁹ Mwangalie yule—yule kuhani, yeye alisema, “Njoo, uweke mkono Wako juu ya binti yangu, naye a—ataamka, atakuwa mzima kama Wewe utakuja na kuweka mikono Yako juu yake.” Hao ni Wayahudi, wekeni mikono.

¹⁹⁰ Lakini alipomjia yule akida wa Kirumi, alisema, “Sistahili Wewe uingie chini ya nyumba yangu, nena tu Neno.” Alitambua nini? Kwamba Yesu alikuwa na nguvu juu ya magonjwa yote. Akasema, “Mimi ni—mimi ni—mimi ni akida,” hao ni watu mia moja, *karne* ni watu mia moja, “Ninamwambia *huyu*, ‘Nenda ukafanye *hivi*,’ naye anafanya, namwambia *huyu*, ‘Njoo,’ naye anakuja, maana hana budi kufanya hivyo, niko juu yake.” Alisema nini, *kiasi hiki*? “Ninajua ya kwamba Wewe uko juu ya kila maradhi, kila ugonjwa, nena tu Neno, hilo tu ndilo unalopaswa kufanya.”

Yesu alisema nini? Aligeuka, akasema, “Sijawahi kuona imani kama hii katika Israeli.”

¹⁹¹ Sasa, tunataka kuwa nayo mahali pa juu zaidi, sivyo? Uponyaji tayari umefanywa pale Kalvari. Sasa, kama Mungu ataleta angalau watu wawili hadi watatu katika kusanyiko hili usiku wa leo ambao sijui lolote kuwahusu, na ataonyesha ya kwamba yale niliyowahubiria ni kweli, kama Yeye atathibitisha tu ya kwamba nimewaambia kweli. . .

¹⁹² Sasa, jifungie tu kwa dakika moja, useme hivi: “Bwana Yesu, mtu huyu hanijui.”

¹⁹³ Sasa, kuna yapata watu wawili au watatu ninaowajua huko nje. Ninawajua Ndugu na Dada Evans walioketi hapa, na hawa ni binti zao wawili walioketi papa hapa. Na halafu Ndugu Sothmann, Ndugu Fred Sothmann pale, ni mmoja wa wadhamini kanisani mwangu huko Jeffersonville. Nami nafikiri Ndugu Simpson, yule ndiye pamoja na mkewe, na Ndugu, Dada Simpson aliyeketi moja kwa moja karibu nao, wamerudi huku kila mmoja.

¹⁹⁴ Sasa, ninataka tu kuliangalia kusanyiko kwa muda kidogo tu, ninawatakeni mwamini kwa moyo wenu wote. Loo, hujui jinsi ambavyo. . . Nilihisi tu ikinigusa wakati uo huo, mnaona, na—najua litatukia, hivyo tu. Mungu ameahidi jambo hilo, ahadi Zake ni kweli. Mtaamini? Niaminini mimi kama mtumishi Wake. Ajabu!

¹⁹⁵ Kama nilivyokuwa nikiwaambia hivi majuzi kuhusu kusimama huko, India, mwajua, mahali hao maelfu walipokuwa, sasa hivyo ndivyo tu ilivyokuwa. Unayo moja kwa moja mkononi mwako, Mungu amekupa moja kwa moja.

¹⁹⁶ Ninachukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu mwenyewe, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Loo, ni kitu gani kingeweza kutukia sasa!

¹⁹⁷ Mnaona, tunafurahi, hiyo ndiyo furaha ya Mungu, hiyo ndiyo furaha ya wokovu wetu. Hiyo ni kweli? Mnaona Daudi kamwe hakupoteza wokovu wake, alisema, “Unirudishie furaha ya wokovu wangu.” Alikuwa na wokovu wake, bali alipoteza furaha yake.

¹⁹⁸ Vema, tuna furaha tele, tunajua hilo, tuna furaha, “Furaha isiyoneneka na iliyojaa utukufu,” tumeipata. Lakini sasa, hicho kitu, nguvu za Mungu ni kitu kikuu kuliko furaha, nguvu huja kwa imani iliyotulia. Tunaweza kuwa na furaha nyingi, lakini labda hatutakuwa na nguvu humo ndani za kuponya hata kidogo. Lakini tunapokuwa na—tukiwa na nguvu za Mungu, basi tuna imani ya Mungu inayopanda juu, inamshika Mungu, inajua jinsi ya kumgusa.

¹⁹⁹ Sasa, iweni tu mkiomba. Ninawaangalia ninyi. Kama atanigusa, basi ninajua.

²⁰⁰ Yupo mtu yeyote hapa ambaye hajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano hii? Hebu tuone mikono yenu. Hujawahi kuwa katika mojawapo ya hii mikutano hapo kabla? Mwanamume mmoja, wanaume wawili, wanaume watatu, wanne, watano, hilo ni jema, sita. Watu sita hawajawahi kuwa ndani yake hapo kabla. Ninataka kuwaambia jambo fulani basi, ndugu, Yesu alipataje kutambu-. . . ulimwengu ulimtambuaaje Yesu kama Masihi? Kwa sababu kwamba Yeye angeweza kuwaambia wao walikuwa ni akina nani, ama kile walichokuwa, ama. . .

²⁰¹ Wakati Simoni Petro alipokuja, mzee mvuvi tu, Akasema, “Wewe ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona,” Petro alimwamini; alipokuja, vema, tulipitia tu Biblia nzima, jana usiku tulipomchukua Zakayo juu ya mti; Bartimayo kipofu, wakati alipomgusa, aligeuka, na kumwambia; yule mwanamke kisimani, yeye. . . alimwambia ilipokuwa shida yake, naye akasema, “Njoni mwone Mtu Ambaye ameniambia mambo niliyofanya! Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi?”

²⁰² Kamwe hakufanya hivyo kwa yeyote wa Mataifa, iliwaendea tu Wayahudi na Wasamaria, maana walikuwa wakimtazamia Masihi. Sasa wao, yapata miaka elfu mbili wametangatanga gizani, lakini sasa Mataifa wamekuwa na siku zao za mafunzo, na sasa wanalipeeta Kanisa sasa. Imefikia mwisho, kama tu vile ilivyokuwa ni mwisho wao, miaka elfu nne, kisha mwisho wao, sasa, ni miaka elfu mbili, maana Yeye anawachukua tu baadhi ya wa—watu, si taifa, watu tu kutoka kwa Mataifa kwa ajili ya Jina Lake, watakuwa na Jina Lake, mnaona, kwa ajili ya Jina. Anawachukua watu kutoka kwa Mataifa, lakini basi anawachukua Israeli kwa taifa.

²⁰³ Lakini Yeye ni Kristo yeye yule, Naye aliahidi kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, jambo alilofanya, Yeye angelifanya tena. Ni wangapi wangependa kuninii. . . wanaoamini ya kwamba yule Malaika wa Mungu kwamba

Yule aliyekutana na Lutu, uh, alikutana na Ibrahimu...? Kamwe hakushuka kwenda kwa Lutu, alibaki na Ibrahimu. Ninyi, mmesoma hadithi hiyo, sasa, mara nyingi?

²⁰⁴ Sasa, kuna wawili wao walioshuka kwenda kwa Lutu, na Mmoja wao... Waliwatoa, ila *Huyu* kamwe hakushuka kwenda, na huyo Ndiye aliyekuwa Bwana Mungu, Elohimu. Naye alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema. Kwanza, Yeye alimtazama Ibrahimu, na kumwuliza Ibrahimu alipokuwa Sara, mke wake.

Kasema, “Yuko hemani nyuma Yako.”

²⁰⁵ Akasema, “Nitakuzuru katika muhula,” muhula wake, zile siku ishirini na nane tena. Alikuwa na umri wa miaka mia moja wakati huo, moja kwa moja kwenye tisini, mke alikuwa na tisini, Ibrahimu alikuwa na mia moja. Kisha akasema... Naye akacheka. Akasema, “Kwa nini amecheka?”

²⁰⁶ Sasa, Yeye alisema hilo lingejirudia tena, nitalifanya tu pande zote mbili, tuone kama ni Mungu yeye yule. Sasa, Mungu wa Mbinguni... Basi angalieni, pamoja na Biblia hii, hebu niseme jambo hili, enyi Wakristo, Biblia hii ikiwa juu ya moyo wangu... .

²⁰⁷ Kuna maskini kutokuamini kunakoingia kisiri, mmoja aliingia jana usiku, akaketi pale ukingoni mwa jukwaa, akaudhuru mkutano, Mungu atalishughulikia hilo. Ulidhani sikujua. Huh! Kamwe usiwazie hilo, Ndugu.

²⁰⁸ Hebu niseme jambo hili huku Biblia ikiwa juu ya moyo wangu: Ninafanya hivi, si kwa onyesho, ninafanya hivi kwa sababu ni kutimiza yale Yesu aliyosema yangetukia.

²⁰⁹ Alipokuja, haikumbidi kuponya, alifanya hivyo kusudi litimie. Hiyo ni kweli? Hili halina... Si lazima afanye jambo hili, bali kwamba lipate kutimizwa, Yeye aliliahidi, ni Neno Lake. Na kwa hiyo Yeye analiruhusu tu kwa sababu ya kulitimiza Neno Lake.

Mungu anaweza kuponya ugonjwa wa moyo? Alifanya hivyo wakati huo, sivyo? Yote yamekwisha sasa.

Sijawahi kumwona huyu mwanamke maishani mwangu, bali ameponywa sasa. Je, hilo linatimiza Neno Lake?

Vema, unasema, “Ndugu Branham, hilo linatimiza nini?”

Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli?

“Vema, nilifikiri ulisema Yeye alikuwa *El, Elah, Elohimu*.”

Hiyo ni kweli.

“Vema, ulisema alikuwa amegeuza mgongo Wake, Naye akagundua kile Sara alichokuwa akifanya.”

Kabisa.

Sasa, mnasema, “Kwani wewe Ndiye?”

La, bwana!

²¹⁰ Huyo ni Yeye kote katika jengo hili. Mnaona? Huyo ni Yeye ndani yako, ni Yeye ndani yangu, bali hana budi kutenda kazi kupitia kwa mtu fulani. Hakuna mmoja wetu anayestahili, tusingeweza kustahili, sisi ni wenye dhambi, bali Yeye alituchagua tu. Ninaamini tulikuwa...ya kwamba karama na miito havina majuto. Ninaamini ya kwamba Mungu alituchagua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Kanisa Lake. Mnaamini hilo? Biblia inasema hivyo. Hiyo ni kweli. “Mpinga-Kristo angewadanganya wote walio juu ya nchi ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.”

²¹¹ Ombeni humu ndani, mahali fulani, ombeni mwone. Loo, ndugu, inatoka kwenu, pia, hapa nyuma. Sasa, ninyi ombeni tu pamoja nami, ndugu, tutaona mahali Malaika yuyo huyo alipo.

²¹² Sasa, chukueni tu wakati wenu, iweni na kicho, tutachukua tu wakati wetu. Tuna muda mwingi, msiwe tu na haraka. Msiwe mkisukumana, ketini tu kimya, msemi, “Bwana Mungu, mtu huyo amenigeuzia mgongo wake. Nami ninajua yeye ni mwanadamu tu, kwa hiyo kama yeye—yeye angenijua angeninii...inabidi iwe ni Wewe ukimwambia, hakuna lingine, kwa sababu mimi ni mgeni niliyeketi tu katika mkutano huu hapa.”

Naam, kuna mwanamke anayenitokea papa hapa sasa, ninamwangelia moja kwa moja.

²¹³ Ninawatakeni ninyi ndugu, angalieni *hapa*. Hivi hamwezi kuiona? Angalieni *hapa*, moja kwa moja ukingoni mwa kitambaa hiki *hapa*. Mnaona *hiki* chekundu? Mnaona? Angalieni *hapa*, mnaona ile Nuru?

²¹⁴ Sasa, kuna mwanamke aliyeketi moja kwa moja nyuma yangu, amefadhaika sana. Ana yabisi kavu, kisha ana shinikizo kuu la damu, anasumbuliwa na mzio, na vema, ana matatizo tu. Sasa, laiti asilikose nitakapogeuka! Jina lake ni Bi. Kahn. Simama, Bi. Kahn, pokea uponyaji wako.

Sasa mnaamini? Mwaminini Mungu, basi.

“Ibrahimu, yuko wapi Sara, mkeo?”

“Hemani nyuma Yako.”

Mnaona ninalomaanisha? Vipi kuhusu baadhi yenu wengine? Je, inaweza kutendeka kwenu? Inaweza kama mtaamini.

Hapa, mnamwona maskini mwanamke huyu aliyeketi papa hapa? Mnaiona hiyo Nuru *hapo* juu tu? Angalieni *hapa*.

²¹⁵ Aliniangalia basi, anaomba. Hajiombe mwenyewe, ni kwa ajili ya mwana. Ndiye uliyekuwa ukiombea, mwanao, sivyo, mama? Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake ni nini?

Utaukubali uponyaji kwa ajili yake? Ugonjwa wa tumbo. Hiyo ni kweli. Amini tu, hivyo tu.

216 Vipi kuhusu mtu fulani katika wilaya hii? Nyote mnaamini nini hapo? Unaamini kwa moyo wako wote? Iweni na imani, aminini tu. Ni wangapi hapa walio wagonjwa, wala hawana kadi ya maombi? Anza tu kuyeyuka ndani yako sasa. Unaona? Unataka maombi, bali huna kadi ya maombi. Vema, hakuna mtu aliye na kadi ya maombi, bila shaka, hiyo ni kweli. Ninaamini walisema kulikuwa na kadi moja ya maombi hapa mahali fulani, labda kutoka kwenye mkutano ama kitu fulani. Iwapo kila mtu ana imani tu sasa, na kutumaini, usiwe na shaka! “Kama unaweza kuamini!”

217 Papa hapa, angalia hapa, wewe hapa kwenye mstari wa mbele, hiyo ngiri, unaamini Mungu ataiponya? Unaamini kwa moyo wako wote? Unaweza kupata ulichoomba.

218 Vipi kukuhusu wewe, bwana, uliyeinamisha kichwa chako hapo? Ilipita juu ya huyo mwanamke, ikaja moja kwa moja kutoka hapo juu ya mwanamume huyu. Wewe ni mhitaji, pia, sivyo? Unaamini ya kwamba Kristo anaweza kukuponya? Una shida na macho yako, na masikio yako. Unatoka Houston, Texas. Bw. West, rudi, ukawaambie huko Houston, Kristo huwaponya wagonjwa.

Unaamini kwa moyo wako wote sasa?

Ulikuwa na ugonjwa wa kuchanganyikiwa, sivyo, mama? Wewe, kutoka kwenye shirika la Corpus Christi kule, amini kwa moyo wako wote.

Mungu ndiye Mponyaji wa mateso yote. Unaamini kwa moyo wako wote?

219 Uliinua mkono wako huko juu, muda mfupi uliopita, bwana, ukiwa na ugonjwa huo wa ini na ugonjwa wa tumbo, Bw. Rainwater, kutoka huko Louisiana. Mara ya kwanza ulipopata kuwa mkutanoni, nafikiri uliinua mkono wako. Unawazia nini juu Yake? Je, Yeye ni Mponyaji wa ajabu? Rudi ukawaambie kule kile anachoweza kukufanyia, kote sasa, mnaona.

220 Aliyeketi nyuma huko nyuma, mvulana huyo mdogo, ana kuziba kwa akili, sivyo? Kulisababishwa na daktari kumfanyia kitu fulani, nusukaputi nyingi kupita kiasi, zikamfanya kuzibika akili. Kama nikikwambia wewe ni nani, utamwekea mkono mvulana huyo kwa niaba yangu? Bibi Howell, hiyo ni kweli, weka mkono wako juu ya mvulana huyo, nitamlaani ibilisi huyo.

221 Shetani, toka ndani yake!

222 Katika Jina la Yesu Kristo, ninauombea uponyaji wake.

223 Mnaamini? Je, kila mtu anaamini? Je, Mungu yupo hapa? Je, hii ndiyo ile chanjo? Je, huyu ni Roho Mtakatifu yeye yule, Bwana Yesu yeye yule, Yule aliyeahidiwa?

224 Ni wangapi wenu walio waaminio? Inua mkono wako. Haleluya! Basi wekeaneni mikono, na mfanye tu kama ninavyowaambia sasa. Sasa tulieni kabisa, wekeaneni mikono. Nina jambo fulani sasa, kama tu utajali hili, kwa dakika moja tu. Vema.

225 Sasa, nitaomba, hakika, ninajua kile kitakachohitajika kumshinda adui wenu sasa, nitaweka maneno kinywani mwako, nawe uyarudie kutoka moyoni mwako. Wewe yaombe, nitayanena:

226 “Bwana Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa milele, Mpaji wa kila karama njema, nisamehe dhambi zangu za kutokuamini, na unipe rehema Yako. Ninakuamini Wewe, ninakukubali kama Mwokozi wangu, wokovu wangu pekee, ninahitaji nguvu Zako kwa ajili ya afya yangu, siwezi kwenda mbele bila Wewe, sasa ninakukubali kama Mponyaji wangu.

227 “Ninamkataa ibilisi na kazi zake zote. Tangu wakati huu na kuendelea, nitawaza mema, nitaamini kila ahadi, yale Maandiko yanayosema, ‘Kwa kupigwa Kwake mimi niliponywa,’ sasa ninaukubali, ninauamini, ni wangu. Ninakushukuru, Bwana. Nitaendelea kushuhudia uponyaji wangu mpaka nitakapokuwa mzima kabisa.”

228 Sasa, sasa tulieni, endeleeni kuwekeana mikono sasa. Sasa ninyi ombeni, sasa jifungieni ndani pamoja na Mungu, mtaona jambo fulani likitukia sasa.

229 Vema, ndugu, wahudumu, kila mtu, mko tayari? Sasa, kama Mungu atayasikia maombi yangu hapa, Yeye huyasikia mahali popote. Sasa, uliomba, umefanya maungamo yako, kama tu vile ungefanya ukija kama Mkristo, uko tayari sasa, kama ulikuwa mwenye dhambi, uko tayari kwa ubatizo, sasa, kwa kuwa wewe ni Mkristo, umefanya maungamo yako, na sasa uko tayari kwa uponyaji. Sasa, inahitaji nini?

230 Sasa, Mungu yuko tayari kukupa wewe, kuna kitu kimoja tu juu yako, hicho ni kivuli kidogo, chembamba cha shaka. Sasa, laiti tungaliweza kupenya kupitia hilo sasa! Ni kama tu ndege kubwa, wananiambia hizi ndege za jeti, kama, zikikakamka tu, na kuyumbayumba, na kukakamka, na kuyumbayumba mpaka zipite kizuizi hicho cha sauti, lakini baada ya kwenda kasi zikapita kizuizi cha sauti, basi ziko huru. Sasa, kama unaweza tu kujiinua juu ya kile kizuizi ki—kidogo cha shaka hapo, loo, ndugu, ni kitu gani kitakachotukia! Utakuwa huru, utaponywa.

231 Sasa, ninawatakeni mwe na kicho kabisa, Shikaneni mikono ninyi kwa ninyi, na mwendeleo kujifungia ndani pamoja na Kristo sasa, kana kwamba hakuna mtu aliye karibu nawe ila Yeye, na uwazie tu moyoni mwako, sasa, unamwona akikushukia moja kwa moja akishuka kuja kwako, amesimama moja kwa moja mbele yako. Sasa fungua moyo wako na umruhusu aingie

ndani, wakati nikiomba na kutupilia mbali kivuli hiki kidogo cha giza juu yako. Basi kitakapovunjika, umetoka kwenye hicho kizuizi cha sauti basi, simama tu na umpe sifa, kila wakati unapohisi nafsi yako imepita kutokuamini huko, basi uko huru katika Kristo.

²³² Baba wa Mbinguni, tukikushukuru kwa yote ambayo umefanya, kwa ajili ya uponyaji mwingi, kwa ajili ya nguvu kuu za Mungu, kwa ajili ya wengi ambao wameokoka, kwa ajili ya ushirika wa wahudumu, na zaidi ya yote, ushirika wa Roho Mtakatifu. Hujatukosea hata wakati mmoja, bali umetwambia ukweli kila wakati, ukathibitisha Neno Lako huku ishara na maajabu yakifuata.

²³³ Na sasa, Baba, kundi hili dogo limeyumbayumba kupitia kwenye barabara hizi zinazoteleza na mvua, usiku wa leo, kuja hapa kumwona Yesu. Tumekuona Wewe, tumekuhisi Wewe, tunajua Wewe uko hapa, tunalo Neno Lako mioyoni mwetu. Wamekiri, wamekiri waziwazi hadharani, kwamba wanaamini, na wamekukubali Wewe kama Mponyaji wao. Sasa nafsi zao zinajitahidi, Bwana, kuvuka kizuizi hicho kidogo pale, kitu hicho kidogo huko ambacho kinawatikisa, “Sijui kama ingekuwa ni mimi? Sijui kama itapotea?” Basi, Ee Bwana, jalia nguvu za Yesu Kristo ziwainue sasa hivi, zivunjilie mbali kizuizi hicho!

²³⁴ Shetani, rudi nyuma, unashindwa vita, simile Kanisa lipite! Katika Jina la Yesu Kristo, Shetani, simama uondoke hapa, ninakuondoa!

²³⁵ Katika Jina la Yesu Kristo, simameni kwa miguu yenu na mdai uponyaji wenu! Dai uponyaji wako, na vizuizi vyote vitaondoka! Ninawakabidhi kwa Bwana Mungu, Yesu Kristo, katika Jina Lake la thamani. Ninatangaza mmeponywa, kila mmoja wenu! Simama na ukubali uponyaji wako sasa, katika Jina la Yesu Kristo. 

61-0125 Kwa Nini?
American Legion Hall
Beaumont, Texas Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org